# Nipashe

Jumanne Juni 9, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580253

www.ippmedia.com

The Guardian digital | nipasheTZ | nipasheTZ | nipasheTZ | 0745 700710




## Wenye malori waomba Tanzania, Kenya kutatua kero za mpakani

UK. 7, 8




UKURASA 11

## URAIS CHADEMA

# Lissu ajinadi kuunda serikali isiyolipa kisasi


- Ataja mambo atakayosimamia, Mchungaji Msigwa naye ajitosa... *Uk. 2*

### BAA LA CORONA



Je? Mtu anaweza kupata Covid-19 kutoka kwenye chakula? Jibu ni kwamba hakuna ushahidi wa hivi karibuni unaonyesha kuwa watu wanaweza kupata ugonjwa huo kupitia chakula. Ugonjwa huo huambukizwa kwa njia ya hewa kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mwingine. WHO

- Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka
- Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana
- Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo



Lissu

Msigwa

## NIMR yafunguka utafiti wa dawa ya Madagascar

UKURASA 2




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play | App Store


## HADHARI YATOLEWA HALI YA HEWA KIPUPWE

UKURASA 3


MICHEZO CHAMA: UBINGWA BARA, FA CUP MUHIMU SIMBA UK.23

MAONI, KATUNI UK.6

# Nimr yaendelea utafiti wa dawa ya Madagascar

**Na Maulid Mmbaga**

TAASISI ya Taifa ya Kupambana na Magonjwa ya Binadamu (Nimr), imesema kuwa inaendelea na utafiti wa dawa kutoka nchini Madagascar, na utakapokamilika utatolewa kwa umma.

Utafiti wa dawa hiyo ulianza baada ya kukabidhiwa Nimr na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, aliyekwenda kuichukua nchini humo mwanzoni mwa Mei, mwaka huu.

Akihojiwa kwenye kipindi cha kumepambazuka kinachorushwa hewani na Radio One, Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi hiyo, Prof. Yunusi Mgaya, alisema kumekuwa na malalamiko ya watu kuhoji kwamba kwanini dawa ya Madagascar haitumiki licha ya kuwapo nchini.

"Dawa hii bado ipo chini ya Nimr kwa uchunguzi zaidi na utakapokamilika itatolewa ili itumike," alisema na kuongeza:

"Nimr jukumu lake ni kupambana na magonjwa ya binadamu kwa maana ya kutengeneza dawa zitakazo dhibiti maradhi yanayotuandama ikiwamo ya mlipuko ili kuhakikisha usalama wa afya, hivyo utafiti ya dawa ya Madagascar utakapokamilika tutaitoa ili wananchi waitumie."

Mkurugenzi huyo alisema dawa lishe ya Nimricaf inayozalishwa na taasisi hiyo yenye uwezo wa kutibu kifua kikavu na mafua makali, mwananchi wa kawaida anaweza kutengeneza nyumbani kwake kwa kufuata vipimo sahihi.

Alisema dawa hiyo ni mchanganyiko wa tangawizi mbichi, pilipili kichaa, kitunguu maji, limao na kitunguu saumu, na kwamba imeshafanyiwa utafiti na kuthibitika inatibu na wapo waliokuwa na corona wameleza kupona.

"Sisi siyo wafanyabiashara, dhumuni letu ni kuwasaidia wananchi na ndio maana tulitoa fomula ya dawa hiyo ili watakaoweza watengeneze wenyewe majumbani mwao ili iwasaidie," alisema.

**JINSI YA KUTENGENEZA**

Prof. Mgaya alisema utengenezaji wa dawa hiyo ni mchanagnyiko wa maji moto lita moja, tangawizi zenye saizi ya kidole ziwe tano, malimao mawili, vitunguu maji vya wastani viwili, vitunguu saumu vidogo vipande 15, na pilipili kichaa nne, ambavyo husagwa kwa pamoja na kulainika kabisa ambayo mtu anaweza kutumia kwa siku nane.




Baadhi ya mabasi yanayotoa huduma ya kusafirisha abiria mikoani na nje ya nchi yakipakia abiria ndani ya kituo kikuu kipya cha mabasi cha Jiji la Dodoma, katika eneo la Nzuguni, jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Lissu atangaza nia kugombea urais

**Na Waandishi Wetu**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Tundu Lissu, ametangaza nia ya kugombea urais kupitia chama hicho huku akiahidi kuunda serikali ambayo haitalipiza kisasi kwa yeyote.

Pia, ametaja mambo ambayo serikali yake itayasimamia ikiwamo kufumua mfumo wa kodi na kufuta sheria kandamizi dhidi ya wananchi.

Lissu ametangaza nia hiyo akiwa ni mwanachama wa tatu tangu chama hicho kifungue milango wiki iliyopita kuruhusu wanachama wake kutangaza nia ya kupeperusha bendera ya chama hicho kwenye uchaguzi mkuu, Oktoba, mwaka huu.

Akizungumza kwa njia ya mtandao kutoka nchini Ubeligiji alikokwenda kwenye matibabu, baada ya kushambuliwa kwa risasi Septemba mwaka 2017, jijini Dodoma, alisema tayari amewasilisha barua ya nia yake kwa Katibu Mkuu wa chama hicho.

Lissu alisema kuna haja ya kuwa na maridhiano ya kitaifa.

"Mwasisi wa taifa la India aliwahi kusema, jicho kwa jicho litatufanya sisi wote kuwa vipofu, makosa mawili hayatengenezi jambo moja la haki kama ambavyo waongo wawili hawatengenezi mkweli mmoja, naamini kwamba matatizo makubwa na ya msingi ya matumizi makubwa ya madaraka, hayawezi kutatuliwa kwa kulipiza kisasi juu ya wale waliotutesa na kutukandamiza."

"Visasi ni upanga wa walio waoga na wadhaifu, siyo ngao ya walio jasiri."

"Kama rais, serikali yangu haitalipiza kisasi ya mabaya mengi ambayo wananchi wetu, mimi mwenyewe na viongozi na wanachama wenzangu wamefanyiwa na utawala huu na hata utawala wa nyuma."

"Badala ya kulipiza visasi, serikali yangu itarudisha, kujenga na kuimarisha mapatano na maridhiano ya kitaifa yatakayojengwa katika misingi ya ukweli juu ya makosa yaliyofanyika, msamaha kwa wanaotubu makosa yao, na fidia kwa wahanga wa makosa hayo."

**ATAJA MAMBO ATAKAYOSIMAMIA**

Lissu aliyewahi kuwa mbunge wa zamani wa Singida Mashariki, alisema endapo atateuliwa na chama chake kuwania nafasi hiyo na kuchaguliwa na wananchi katika uchaguzi ujao wa Oktoba, kwanza serikali yake itaandaa sera thabiti za kiuchumi zitakazohakikisha serikali inabaki mwangalizi wa shughuli za kiuchumi zinazoendeshwa na sekta binafsi.

Pili, alisema serikali yake itakuwa msimamizi wa maslahi ya jumla ya wananchi ili kuhakikisha usalama wa bidhaa na udhibiti wa bei za bidhaa na huduma muhimu kwa ustawi wa wananchi.

Tatu, atafanya mageuzi makubwa ya mfumo wa utozaji kodi kwa kuondoa utitiri wa kodi unaochangia kuangamiza mitaji ya wafanyabiashara na wajasiriamali.

Nne, serikali yake itafanya mageuzi makubwa ya mfumo mzima wa vyombo vya ulinzi na usalama, ili kuvifanya kuwa walinzi wa Katiba, haki za binadamu na uhuru wa wananchi kufanya shughuli zao kwa mujibu wa Katiba.

Tano, atatii, kulinda na kuhifadhi mfumo wa vyama vingi vya siasa na kuondoa vikwazo.

"Mazuio ya mikutano ya hadhara na maandamano ya kisiasa ya wananchi, wawe kwenye vyama vya siasa au katika taasisi zao nyingine yataondolewa," alisema Lissu.

Vile vile, alisema atarudisha hadhi, heshima na madaraka ya bunge kama muhimili mkuu wa dola wenye mamlaka yanayolingana na serikali ndani ya mipaka yake.

Lissu anakuwa mwanachama wa tatu kutangaza nia ya kuwania urais baada ya Mbunge wa Iringa Mjini, Mchungaji Peter Msigwa, kutangaza nia ya kutaka kugombea urais kupitia chama hicho, Ijumaa iliyopita.

Mchungaji Msigwa ambaye ni Mwenyekiti wa Chadema Kanda ya Nyasa, aliwasilisha barua yake ya kutangaza nia kwa Katibu Mkuu wa Chadema, John Mnyika, mwishoni mwa wiki.

Kada mwingine wa Chadema aliyetangaza kuwania urais ni Dk. Maryrose Majinge, ambaye aliwahi kujitokeza kuwania nafasi ya ubunge katika Jimbo la Ukonga mwaka 2015 na kushindwa na Naibu Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) Mwita Waitara.

Licha ya vigogo waliotangaza nia ya kutaka kuteuliwa na Chadema kuwania nafasi hiyo ya juu kabisa nchini, Dk. Majinge, alinukuliwa akidai anajiamini na kuwa hakuna kigogo anayemuhofia kushindania naye nafasi hiyo.

***Imeandikwa: Mary Geofrey na Elizabeth Zaya***


## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliopewa na **HARBOR MICROFINANCE COMPANY LIMITED.** Sisi **J.J RECOVERY** tunatoa taarifa kwa wadaiwa wote kulipa deni unalodaiwa ndani ya siku 14 ya tangazo hili baada ya hapo tutapiga mnada dhamana (nyumba) za wateja zilizo orodheshwa hapo chini:

| | JINA | AINA YA DHAMANA | MAHALI ILIPO DHAMANA | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | PILI FOCUS SILAYO | NYUMBA | CHAMANZI, MTAA WA RUFU | KUANZIA 22/06/2020 NA KUENDELEA |
| 2 | DONALD M. BISEKO | NYUMBA | GOBA, MTAA WA KINZUDI | KUANZIA 22/06/2020 NA KUENDELEA |
| 3. | OBONYO L. SEDA | NYUMBA | MWANDEGE, KITONGOJI CHA CHATEMBO | KUANZIA 22/06/2020 NA KUENDELEA |

**Kwa mawasiliano wasiliana na: J.J RECOVERY kwa namba 0714 292260 / 0784 076588.**



Wananchi wakipita kwenye daraja linalounganisha vijiji vya Bulinga, Bugunda na Bwasi katika Wilaya ya Musoma, mkoani Mara juzi, ambalo serikali imelitengea Sh. milioni 300, kwa ajili kulitengeneza upya ili liwe imara zaidi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**.

# TMA yawataka wadau kuchukua tahadhari

**Na Faustine Feliciane**

MAMLAKA ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), imetoa rasmi mwelekeo wa hali ya hewa wa msimu wa kipupwe nchini, unaoanzia mwezi Juni hadi Agosti na kuwataka wadau kuchukua tahadhari wanapotekeleza majukumu yao kwa kufuata utabiri wa hali ya hewa.

Mkurugenzi Mkuu wa TMA, Dk. Agnes Kijazi, akitangaza hali hiyo aliwataka wananchi kufuatilia utabiri huo wa msimu wa kipupwe kwa kipindi cha Juni hadi Agosti (JJA) 2020, kuwapo kwa mvua za msimu wa Machi hadi Mei ambazo zilileta athari hapa nchini zimeisha.

"Msimu huu wa kipupwe unatarajiwa kuwa na vipindi vifupi vya upepo mkali wa kusi na hali ya ukavu katika maeneo mengi ya nchi, hata hivyo, vipindi vya baridi kali vinatarajiwa katika maeneo ya miinuko ya nyanda za juu kusini-magharibi hususan nyakati za usiku na asubuhi," alisema Dk. Kijazi na kuongeza,

"Vipindi vya baridi kali vinatarajiwa hasa katika wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Juni na kupungua kuelekea mwishoni mwa msimu yaani mwezi Agosti kwa maeneo ya mikoa ya Mbeya, Songwe, Njombe na Rukwa pamoja na baadhi ya maeneo ya mkoa wa Ruvuma, maeneo haya yanatarajiwa yatakuwa na joto la kawaida kati ya nyuzi joto 6 na 12, hata hivyo baadhi ya maeneo hususan katika mikoa ya Njombe na Mbeya yanatarajiwa kuwa na joto la chini ya nyuzi joto 6," aliongezea Dk. Kijazi.

"Nawakumbusha wananchi kuchukua tahadhari na kufuatilia utabiri wa saa 24, siku 10 pamoja na mwezi kama unavyotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania," alisisitiza Dk. Kijazi.

Dk. Kijazi ambaye ni Makamu wa Tatu wa Rais wa Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO), alielezea hali ya joto katika maeneo mengi hapa nchini, huku akibainisha kuwa joto la kawaida linatarajiwa katika maeneo mengi ya ukanda wa pwani na kuashiria uwapo wa vipindi vichache vya baridi ikilinganishwa na hali ya wastani wa muda mrefu (1981-2010) kwa miezi ya Juni hadi Agosti katika maeneo hayo.

# CUF yafungua pazia udiwani, ubunge

**Na Salome Kitomari**

CHAMA cha Wananchi (CUF), kimeanza mchakato wa ndani wa kuruhusu wenye nia ya kugombea ubunge na udiwani kuchukua fomu na kuzirejesha ndani ya mwezi huu.

Akizungumza jana na Nipashe kwa njia ya simu, Naibu Katibu Mkuu Bara, Magdalena Sakaya, alisema wakati wanasubiri majibu ya barua kutoka kwa Msajili wa Vyama vya Siasa nchini, namna vyama vitakavyoendesha shughuli zake wakati wa zuio la mikusanyiko kutokana na janga la corona, wataendelea na mchakato wa ndani.

Alisema uchukuaji wa fomu umeanza Juni 6 na utaendelea hadi mwishoni mwa mwezi, kwa watia nia kujaza na kuzirejesha wilayani na kwamba kura ya maoni itafanyika mapema Julai.

"Kura ya maoni inahitaji kukutanisha wanachama wengi kwa wakati mmoja na hadi sasa hakuna majibu ya barua yetu kutaka ufafanuzi wa kuhusu mikusanyiko, wanachama wetu wanatuuliza kila mara kwa kuwa wanataka kujua wanawezaje kuendelea kujipanga ikiwamo kuzungumza na wanachama ili kuwashawishi wapate ridhaa ya kupeperusha bendera ya chama," alisema.

Kuhusu wito wa ushirikiano uliotolewa na vyama vya Chadema na NCCR- Mageuzi, Sakaya alisema Juni 22, watakutana kujadili suala hilo na kutoa uamuzi wa pamoja.

"Ili ukubali kushirikiana ni lazima ufanye maandalizi ya ndani ambayo ni muhimu sana, hivyo tutajadiliana kushirikiana baada ya kukamilisha mchakato wa ndani, kwa sasa Mwenyekiti wetu, Prof. Ibrahim Lipumba, yupo visiwani Zanzibar kikazi baada ya kurejea tutakuwa na mfululizo wa vikao," alibainisha.

Sakaya ambaye ni Mbunge wa Kaliua, alisema kuchelewa kutolewa kwa ruhusa ya mikutano kunavifanya vyama kushindwa kupanga ratiba zao kikamilifu ikiwamo mipango ya kibajeti.

"Kwa sasa tumepanga ratiba zetu, lakini ziko vipande vipande kwa kuwa bado hatujapata kauli ya serikali kuhusu zuio la mikutano la tangu mwaka 2015, kutokana na janga la corona, pia tunashindwa kupanga bajeti zetu, tunawaomba watoe kauli ili tuweze kuendelea na ratiba zetu," alisema.

Uchaguzi mkuu wa diwani, mbunge na rais unatarajiwa kufanyika Oktoba 30, mwaka huu.

Rais atavunja Bunge Juni 19, mwaka huu, na baada ya hapo mchakato wa uchaguzi mkuu utaanza kwa kuwa kutakuwa hakuna madiwani wala wabunge, na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), itatoa ratiba ya uchaguzi mkuu ikiwamo tarehe rasmi ya kuanza kampeni.

Hadi sasa kuna vyama 19 vyenye usajili wa kudumu, na hivi karivuni Chadema ilitangaza kuruhusu wanachama wake kutia nia ya kugombea urais, ushirikiano na vyama vingine vya upinzani vyenye nia ya kuing'oa CCM madarakani, jambo ambalo lilitangazwa na NCCR-Mageuzi pia.

Juzi, ACT-Wazalendo kilitangaza kukubali kushirikiana na Chadema na tayari wameandika barua, ambayo chama hicho kilithibitisha kuipokea na kueleza kuwa katika wakati muafaka kitatoa taarifa ya hatua zinazoendelea.

# NBS: Mfumuko wa bei umepungua kwa asilimia 3.2

**Na Augusta Njoji**, DODOMA

OFISI ya Taifa ya Takwimu (NBS), imesema mfumuko wa bei wa Taifa kwa mwaka ulioishia Mei, 2020 umepungua hadi asilimia 3.2 kutoka asilimia 3.3 kwa mwaka ulioishia Aprili, 2020.

Hayo yalibainishwa jana na Kaimu Mkurugenzi wa Sensa ya Watu na Takwimu za Jamii wa Ofisi hiyo, Ruth Minja, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu hali ya mfumuko wa bei nchini.

Alisema kupungua kwa mfumuko kunatokana na mabadiliko ya bei za baadhi ya bidhaa na huduma.

"Kupungua kwa mfumuko wa bei kwa mwaka ulioishia Mei, 2020 kumechangiwa na kupungua kwa bei za baadhi ya bidhaa za vyakula na bidhaa zisizo za vyakula kwa kipindi kilichoishia Mei, 2020 zikilinganishwa na bei za Mei, 2019," alisema.

Minja alisema baadhi ya bidhaa za vyakula zilizopungua bei mwezi Mei, 2020 zikilinganishwa na bei kwa mwezi Mei, 2019 ni pamoja na matunda kwa asilimia 5.8, viazi mviringo kwa asilimia 5.5, mihogo kwa asilimia 13.9, viazi vitamu kwa asilimia 8.8 na ndizi za kupika kwa asilimia 3.

"Kwa upande mwingine baadhi ya bidhaa zisizo za vyakula zilizopungua bei kwa mwezi Mei, 2020 zikilinganishwa na bei za mwezi Mei, 2019 ni mafuta ya taa kwa asilimia 14.3 petroli kwa asilimia 10 na dizeli kwa asilimia 12.9," alisema.

Aidha, alisema mfumuko huo wa bidhaa za vyakula na vinywaji baridi kwa mwaka ulioishia mwezi Mei, 2020 umepungua hadi asilimia 4.4 kutoka asilimia 4.6 kwa mwaka ulioishia mwezi Aprili 2020.

Kwa upande wa nchi za Afrika Mashariki, Mkurugenzi huyo alisema Kenya mfumuko kwa kipindi hicho umepungua hadi kufikia asilimia 5.47 kutoka asilimia 5.62 kwa mwezi Aprili, 2020.

"Kwa Uganda, mfumuko wa bei kwa mwaka ulioishia mwezi Mei, 2020 umepungua hadi asilimia 2.8 kutoka asilimia 3.2 kwa mwaka ulioishia Aprili, 2020," alisema.

Akizungumzia mabadiliko ya fahirisi za bei, alisema kati ya mwezi Aprili na Mei mwaka 2020, yameongezeka kwa asilimia 0.2 na limechangiwa na kuongezeka kwa bei kwa baadhi ya bidhaa za vyakula na visivyo vya vyakula ikiwamo suti, magauni na gharama za saluni kwa wanawake.

Alitaja bei zingine zilizochangia ongezeko hilo kwa upande wa vyakula ni mtama kwa asilimia 4.1, samaki kwa asilimia 3, dagaa kwa asilimia 1.2, karanga kwa asilimia 2.2, maharage kwa asilimia 5.7, mihogo kwa asilimia 2.6 na ndizi za kupika kwa asilimia 4.4.

Kwa upande wa bidhaa zingine zisizo za vyakula, alisema ni bidhaa za usafi wa kaya kwa asilimia 1.1, mavazi ya wanaume kama suti kwa asilimia 1.1, mavazi ya wanawake kama magauni kwa asilimia 1.3, kuni kwa asilimia 3, madaftari kwa asilimia 1.8 na gharama za saluni kwa wanawake kwa asilimia 1.1.

# Lwakatare hajasahau balaa mchuano ubunge na Kagasheki

- Akumbusha kikosi cha Meya Ruhangisa
- Kura 148 za Lwakatare 'aterwe' zilimng'oa
- Aanika chanzo kuhama CUF kwenda Chadema

Na Sanula Athanas, DODOMA



**JANA katika sehemu ya kwanza ya mazungumzo ya faragha na Nipashe, mwanasiasa mwandamizi na Mbunge wa Bukoba Mjini anayestaafu, Wilfred Lwakatare, alifunguka shinikizo lililomng'oa jukumu la Ofisa Utumishi serikalini, akawa mwanasiasa mtetezi wa wafanyakazi hadi ubunge.**

Lwakatare (56), ambaye amewahi kuwa Mkurugenzi wa Idara ya Ulinzi na Usalama wa Viongozi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), alikumbusha namna alivyolazimika kuilipa serikali mishahara ya miezi mitatu ndani ya saa 24 ili kufanikisha malengo yake ya kisiasa.

Leo katika sehemu ya pili ya mahojiano haya, mbunge huyo ana simulizi za joto la uchaguzi mkuu wa mwaka 2005, alipochuana vikali na timu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM). Fuatilia maelezo yake:

**SWALI: Ninakumbuka mwaka 2005, CCM walikupania kwelikweli, walijikusanya wengi wakiwa katika siasa za Lwakatare 'aterwe' (maana yake apigwe). Unaukumbukaje mchuano wako na Kagasheki?**

**LWAKATARE:** Uchaguzi wa 2005 ulikuwa wa mchuano mkali kwelikweli, nguo kuchanika.

Nilikuwa nimemaliza kipindi changu cha kwanza cha ubunge lakini pia nimemaliza nikiwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni (KUB).

Wakati huohuo nilikuwa pia Naibu Katibu Mkuu wa Chama cha Wananchi (CUF). Kitaswira, katika medani za kisiasa, nilikuwa nang'ara kisawasawa.

Kuja kwa Kagasheki miaka mitatu kabla ya uchaguzi na kuanza kutambulishwa kinamna na mamlaka ya mji, chini ya mwanasiasa mkongwe mzoefu marehemu Samwel Ntambala Ruhangisa, akiwa mstahiki meya wa mji, kulikinusuru Chama Cha Mapinduzi kisipigwe mwereka mwingine.

Kagasheki aliingia katika uchaguzi huo akiwa na ukwasi wa kutosha. Alikuwa ametokea kwenye ofisi za kitengo cha Oil for Food cha kuisaidia Iraq chakula wakati wa vita yake na Marekani.

Kwa wenye kufuatilia matukio makubwa ya siasa za kidunia na migogoro ya UN (Umoja wa Mataifa), mradi huo uliibua kesi kubwa iliyomhusisha mtoto wa Katibu Mkuu wa zamani wa UN, juu ya 'deal' kubwa ya utakatishaji fedha zaidi ya Dola bilioni 19 za kimarekani.

Kesi hiyo ililihusisha dawati lililokuwa kwa namna fulani... Balozi Kagasheki pia aliitwa katika kesi hiyo na mahakama za Uswisi. Nyaraka zimo mitandaoni kuhusiana na suala hilo.

Kipindi cha miaka mitatu kabla ya uchaguzi, Balozi Kagasheki alipewa fursa ya kufadhili miradi ya fedha nyingi ndani ya Manispaa ya Mji wa Bukoba.

Mambo mengi makubwa yaliyotokea katika uchaguzi huo, lakini pamoja na vituko vyote, ndani ya uchaguzi huo, Balozi Kagasheki alitangazwa mshindi kwa tofauti ya kura 148 dhidi yangu.

**SWALI: Tupate kwa kina leo, kulitokea nini tena ukatimkia Chadema?**

**LWAKATARE:** Nitajitahidi kuyaeleza yanayoelezeka kwa sasa na mengine nitakuja kuyaongezea kwenye majibu siku za mbele. Sikupenda kamwe kutoka ndani ya CUF, lakini mambo ya sintofahamu yalijitokeza.

Ilifikia mahali ikanilazimu kutoka, ili kuilinda heshima yangu lakini pia kujijengea mazingira mazuri ya kisiasa ambayo yangefuata baada ya hapo.

Sababu kubwa ya kutoka CUF ninayoweza kuitoa hapa, ni siasa za fitina, uongo, uzandiki, wivu, tamaa, majungu, ubabaishaji, kutojitambua na uelewa mdogo wa mambo ya kisiasa kwa baadhi ya viongozi waliokuwa na nyadhifa mbalimbali ndani ya CUF.

Viongozi hao walipinga mitizamo yangu mingi, hoja, dira na mifumo ya kiuongozi na kiutawala ndani ya chama. Mfano; pamoja na ukweli kwamba kipindi hicho CUF kilikua chama kikuu cha upinzani, kwa mwelekeo wa kisiasa ulivyokuwa ukionekana kwa siku zilizokuwa zinajionyesha mbele, Chadema kilikuwa kinaonekana kukua kwa kasi na kingelichukua nafasi ya CUF.

Hivyo, niliwashauri viongozi wenzangu wa CUF tujenge mazingira rafiki ya kuwezesha ushirikiano wa kivyama (vyama vya upinzani) kuwapo, ili kukinusuru CUF na upepo wa Chadema uliokuwa unakuja.

Mtazamo wangu huo tayari nilikuwa nimeanza kuutengenezea 'road map' ya kuifikia, nikiwa nimependekezwa na kuchaguliwa kuwa mwenyekiti wa kamati ya ufundi ya kusimamia na kutengeneza mfumo na utaratibu ambao ungelitumika katika kuviunganisha vyama vyote vya upinzani ambavyo vingeliukubali ushirikiano huo.

Baadhi ya viongozi walifikia hatua ya kunituhumu kwamba ninataka kuiua CUF na kuipaisha Chadema. Ilifikia mahali baadhi ya viongozi, wengi wao wameishahamia vyama vingine au kuanzisha vyama vipya, wakawasilisha 'fake recorded tape', eti nikiwa ninafanya maongezi, yaani makubaliano ya kuimaliza na mimi kuhamia Chadema.

Jambo la pili, ilikuwa hoja yangu ya kupinga namna mapato ya chama yalivyokuwa hayagawiwi kiusawa kwa kutoangalia ukubwa wa maeneo yetu yanayopaswa kuangaliwa na kuhudumiwa na chama.

Zanzibar waliokuwa wanapewa gawio la asilimia karibu 70 na Bara ambayo ni kubwa ikiambulia 30 tu. Hili nililipinga waziwazi ndani ya vikao lakini kutokana na mfumo uliokuwa umejengwa kimkakati ndani ya chama, sikuweza kupenya.

'Notion' ya kuipa Zanzibar gawio kubwa ambalo pia Profesa Lipumba alikuwa akiiamini ilikuwa ni kwamba, ili tuishinde CCM, ni vyema tupeleke nguvu kubwa Zanzibar ambako mfumo wetu wa CUF ulikuwa umeimarika sana, na hivyo tungeliweza kuipata Serikali ya Zanzibar kwanza na kutoka huko Bara tukapewa nguvu na serikali yetu ya CUF Zanzibar na tukawashughulikia CCM Bara na kuichukua dola ya Tanzania Bara pia.

Badala yake mimi nilipinga kwa hoja kwamba kitendo cha kukinyima chama nguvu huku Bara na kuziweka zaidi upande wa Zanzibar tu kingekinyima chama chetu Bara na kuibana CCM isiweze kuhamishia nguvu kubwa Zanzibar.

Kwa njia hiyo, wenzetu Zanzibar wangelipata ahueni ya kutonyang'anywa ushindi. Hawakunisikiliza, wakafanya hayo waliyoyaamini na matokeo yake wao kukutana na niliyoyafikiria na kuyasema vikaoni.

Nilipoona ninatwanga maji kwenye kinu na nikiunganisha na ushawishi mkubwa kwangu aliokuwa akiufanya rafiki yangu sana na rafiki wa familia Mheshimiwa Mbowe (Mwenyekiti wa Chadema) wa mimi kujiunga Chadema, akiwa amenijibu hoja zangu mbalimbali zilizokuwa zikinitia hofu kujiunga na Chadema, baadhi akiwa anajua alinidanganya, nilijiunga kwa moyo mweupe kabisa kwa kufikiri nitatimiza na kuyashuhudia matamanio yangu yaliyonifanya niamue kuacha kazi na kujiunga na siasa.

**USIKOSE KESHO KUFUATILIA MFULULIZO WA MAZUNGUMZO HAYA YA FARAGHA**

# TANGAZO

## DEPOSIT INSURANCE BOARD

### TANGAZO KWA UMMA

**KATIKA SHAURI LA FBME BANK LIMITED (ILIYO CHINI YA UFILISI)**

Taarifa inatolewa kwa umma na Deposit Insurance Board (DIB) kuwakumbusha wenye amana wa iliyokuwa FBME BANK LIMITED kwamba;

1. Zoezi la ulipaji wa fidia ya bima ya amana kwa mujibu wa sheria kwa wale ambao bado hawajalipwa fidia linaendelea kupitia yaliyokuwa Makao Makuu ya FBME Bank Limited yaliyopo Kinondoni, Dar es salaam.
2. Hadi mwisho wa Aprili, 2020, Deposit Insurance Board imelipa fidia kwa asilimia 51.77% ya wateja wanaostahili fidia na asilimia iliyobakia bado hawajajitokeza kuchukua fidia hiyo.
3. Kwa tangazo hili, Deposit Insurance Board inarudia kuwakumbusha wateja wote ambao hawajachukua fidia ya bima ya amana, kufika kwenye yaliyokuwa Makao Makuu ya FBME Bank Limited yaliyopo Kinondoni, Dar es salaam ili kulipwa fidia zao.

**UKISIKIA TANGAZO HILI TAFADHALI MTAARIFU NA MWENZIO.**

**TANGAZO HILI LIMETOLEWA TAREHE 28 MEI 2020**

MKURUGENZI
DEPOSIT INSURANCE BOARD
JENGO LA MAKAO MAKUU YA
BENKI KUU YA TANZANIA
2 MTAA WA MIRAMBO
GHOROFA YA 11,
MNARA WA KASKAZINI
11884 DAR ES SALAAM

BARUA PEPE: DIB-INFO@BOT.GO.TZ
SIMU YA MEZANI: +255 22 223 5390
Fax: +255 22 223 4200

## DEPOSIT INSURANCE BOARD

### TANGAZO KWA UMMA

**KATIKA SHAURI LA MBINGA COMMUNITY BANK PLC, COVENANT BANK FOR WOMEN (T) LTD, EFATHA BANK LTD, KAGERA FARMERS COOPERATIVE BANK LIMITED, MERU COMMUNITY BANK NA NJOMBE COMMUNITY BANK LIMITED (ZILIZO CHINI YA UFILISI)**

Taarifa inatolewa kwa umma na Deposit Insurance Board (DIB) kuwakumbusha wenye amana wa zilizokuwa;

1. **Mbinga Community Bank Plc,**
2. **Covenant Bank for Women (T) Ltd,**
3. **Efatha Bank Ltd,**
4. **Kagera Farmers Cooperative Bank Limited,**
5. **Meru Community Bank Limited na**
6. **Njombe Community Bank Limited, kwamba;**

1. Zoezi la ulipaji wa fidia ya bima ya amana kwa mujibu wa sheria kwa wale ambao bado hawajalipwa fidia linaendelea kupitia matawi yote ya benki ya TPB Bank Plc yaliyopo nchini.
2. Hadi mwisho wa Aprili, 2020, Deposit Insurance Board imelipa fidia kwa asilimia 37.91% ya wateja wanaostahili fidia na asilimia iliyobakia bado hawajajitokeza kuchukua fidia hiyo.
3. Kwa tangazo hili, Deposit Insurance Board inarudia kuwakumbusha wateja wote ambao hawajachukua fidia zao kufika kwenye tawi lolote la benki ya TPB Bank Plc ili kulipwa fidia zao.

**UKISIKIA TANGAZO HILI TAFADHALI MTAARIFU NA MWENZIO.**

**TANGAZO HILI LIMETOLEWA TAREHE 28 MEI 2020**

MKURUGENZI
DEPOSIT INSURANCE BOARD
JENGO LA MAKAO MAKUU YA
BENKI KUU YA TANZANIA
2 MTAA WA MIRAMBO
GHOROFA YA 11,
MNARA WA KASKAZINI
11884 DAR ES SALAAM

BARUA PEPE: DIB-INFO@BOT.GO.TZ
SIMU YA MEZANI: +255 22 223 5390
Fax: +255 22 223 4200

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# *Huenda tunakosea hebu tutafakarini*

**DAR ES SALAAM** ni moja, hivyo na kwenye vita hii ya corona tunahitaji kuwa wamoja na si kupishana katika mikakati ya kuwakinga wananchi na maradhi haya.

Tunasema haya kwa sababu tunaona kama kuna kupishana wengine wanakwenda kwenye taratibu na miongozo ya kukwepa ama kujiepusha na maambukizo wakati wapo wasiofahamu kuhusu kinachoendelea.

Tunasema haya kwa sababu tumekuwa tukipokea maelezo mbalimbali kuhusu kujiepusha na corona na la msingi ni kwa kuwahimiza wananchi kunawa mara kwa mara na kuvaa barakoa.

Hivi karibuni tulifanya uchunguzi kidogo kwenye mabasi ya abiria na kugundua kuwa abiria haruhusiwi kupanda kwenye mabasi yaendayo haraka au mwendokasi bila kuvaa barakoa.

Madereva wa mabasi haya ni wasimamizi wa abiria. Iwapo atatokea asiye na barakoa wanamrudisha au kuwakatalia wasiovaa kuingia ndani ya vyombo hivyo.

Si hivyo tu, hata kwa madereva wa mabasi yanayosafiri kati ya Posta, Gerezani kwenda Tegeta Nyuki na maeneo mengine wanasisitiza uvaaji wa barakoa na wakati mwingine polisi wa usalama barabarani wanapanda na kuwahimiza watu kutumia barakoa.

Abiria wengi wasiotumia njia zinazofika katikati ya mji hawa barakoa wala hakuna anayewahimiza kufanya hivyo licha ya kwamba ni jiji moja na mikakati ya kujiepusha na corona ni ya aina moja.

Tunaomba kama ni suala la kujihadhari na corona jitihada na mikakati iwe ya pamoja na shirikishi kwani lengo ni kuwaokoa wana Dar es Salaam.

Ingependeza kama kungekuwa na mikakati ya pamoja ya kuwaepusha wananchi na maradhi haya ambayo ni hatari na yanayosambaa kwa kasi kubwa na kuua wengi.

Kuna taasisi pia ambazo husisitiza kuwa hakuna kupata huduma wala kuingia kwenye majengo yao iwapo mteja au mhusika hajavaa barakoa.

Ni wazi kuwa mgonjwa hawezi kuingia hospitalini hata iwe ya rufani ikiwa hatavaa barakoa na pia hatahudumiwa kama hana kinga hiyo. Yote haya yanahamasisha kujikinga na kuwalinda wengine na corona.

Ni wazi kuwa katika benki ni vigumu kuingia ama kupata huduma iwapo mteja hajavaa barakoa.

Kwa kuliona hilo kuna haja ya kuamua sasa kuwa hatua hizo zinachukuliwa kila mahali na kwa watu wote. Jukumu hilo lifanyike kwa pamoja na kwa utaratibu unaofanana.

Tunaona kuwa haina maana wengine kujilinda na kundi kubwa kuachwa kufanya wanavyopenda kwa kuwa lengo ni kuokoa maisha ya wote.

Mathalani, askari wa usalama barabarani wanawahimiza abiria wanaoingia na kutoka Kariakoo au Posta kwenye daladala kuvaa barakoa muda wote.

Lakini, hakuna anayejali kuwasimamia abiria wanaosafiri kati ya Mbezi na Mlandizi au Mbezi na Temeke, au Tandika pengine na Makabe iwapo wana barakoa.

Si hivyo askari hao pamoja na mamlaka nyingine hazionekani kuhoji kwanini wasafiri hao wanajazana kwenye magari wengine wakikalia vigoda, ndoo na vibao badala ya kusimamia utaratibu idadi ya viti kwa idadi ya abiria au 'seat level.'


Tunaomba juhudi za kuwakinga wananchi na maradhi zifanyike kwa kuangalia pande zote na kuelimisha watu wote kwa kuwa ni muhimu wawe salama na waepushwe na maradhi.

Hata katika nyumba za ibada ni muhimu pia kuwahimiza watu kuchukua tahadhari na kusimamia afya na usalama kama ambavyo kwenye benki, hospitali na ofisi nyingine hairuhusiwi kuingia bila barakoa ili kujikinga na kuwakinga wenzako.

Tunaamini kuwa Dar ni moja na pia Tanzania ni ya wote hivyo tushikamane ili kuishinda corona.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# *Lukuvi ameacha alama isiyofutika*



Na Salome Kitomari

**UPO** usemi kuwa mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni, hili halina ubishi kwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Willium Lukuvi. Ni miongoni mwa viongozi ambao wamepewa eneo na wamelisimamia kwa weledi.

Kila ukifungua mitandao ya kijamii na hasa Utube unakutana na video za Lukuvi akieleza mambo mbalimbali ya ardhi ambayo yanagusa maisha ya watu na hasa waliopora haki zao na wenye nguvu ya fedha na mamlaka.

Kwenye eneo la ardhi dhuluma, uonevu na mengine mabaya yalitawala kiasi cha watu kudai haki zao mahakamani na njia nyingine kwa miaka mingi bila mafanikio.

Dhuluma mojawapo ni kula njama baina ya madalali na taasisi za mikopo au watu binafsi ambao hukimbilia kuuza mali za watu hasa ardhi na kubadilisha umiliki kwa haraka bila kujali kuwa wanawaachia maumivu makali waliopowa mali zao.

Mathalani, kuna wakati vyombo vya habari vilitawaliwa na habari za mtu mmoja aliyeporwa haki yake kwa kuchukua ghorofa lake na rafiki yake ambaye alishirikiana na watumishi wa idara ya ardhi kutengeneza hati feki.

Kama siyo Waziri Lukuvi ambaye ameamua kusaidia wahitaji, mhusika huyo huenda asingerejeshewa mali yake hiyo.

Nyingine ni mkoani Arusha ambako kuna taarifa za mama mzee kunyang'anywa mali yake na kwa zaidi ya miaka 30. Alidai mahakamani bila kufanikiwa, lakini Waziri Lukuvi, amempa bibi huyo mali yake.

Huenda ardhi ni moja ya maeneo yenye ugumu na lililojaa wajanja wenye kushirikiana na madalali ambao miaka mingi wanakula kwa jasho la wengine kwa kushirikiana na watumishi wasio waaminifu wa Idara ya Ardhi.

Yote haya ni uonevu dhidi ya wananchi ambao wanakesha kwenye mabaraza ya ardhi kusaka haki yao kwa gharama kubwa, lakini wasiipate kutokana na ukweli kuwa waliopo kwenye mfumo wanashirikiana na wanaowanyanyasa raia.

Kwenye miji na majiji kuna kesi nyingi za watu kuporwa ardhi zao, wamiliki wawili kuwa na hati, na wengine kujeruhiwa au kufanyiwa ubaya licha ya kuwa ni haki yao.

Tangu kuingia madarakani kwa Waziri Lukuvi siku zote anatembea huku na kule kupambana na uhalifu huo uliokuwa umeshika atamu, na amefanikiwa kwa kiasi kikubwa kwa kuhakikisha wenye haki zao wanazipata.

Mfano mtu anamiliki ardhi yake tangu miaka ya 90 na ana hati, lakini ghafla anatokea mwingine naye ana hati ya miaka ya 2000 hapo haihitajiki elimu ya sheria kujua nini kilifanyika hadi eneo la mwingine likamegwa pasipokuwa na mauziano yoyote.

Kwa sasa eneo la ardhi linaogopeka kufanya vinginevyo kwa kuwa wanajua iwapo itajulikana hatua zitachukuliwa dhidi ya muhusika.

Kila siku yanaibuka mapya katika sekta hiyo na yote yamevaa sura ya uonevu dhidi ya watu wengi wanyonge wakiwamo wanawake, wajane, yatima na wazee.

Kwa maeneo ya ardhi ambayo ni muhimu sana kiuchumi, nako ukifuatilia kwa kina waliojipatia maeneo hayo ni watu wenye nguvu ya fedha ambazo wamezitumia kuwapora kinyemela.

Naamini Waziri huyu akipewa nafasi na kuendelea kuchapa kazi kama anavyofanya Tanzania itapiga hatua kubwa kwenye kumaliza migogoro ya ardhi ambayo mingi inatengenezwa kwa manufaa ya wachache.

Kwa kuwa mipango miji mingi nchini ilipangwa kabla ya ongezeko la watu na mabadiliko makubwa ya kimaendeleo, ipo haja ya kufanyika kwa mipango mipya ya kupanga mjini na majiji na hasa kwenye maeneo mapya ambayo bado hayajaendelezwa.

Kwa kazi kubwa anayofanya Waziri Lukuvi ni wazi kuwa amejitengenezea maadui ambao walipora haki za watu na kwa kuwa wana fedha wanaweza kufanya lolote wakati wowote.

Kwa misingi hiyo ni vyema zikafanyika jitihada za kumlinda kwa namna yoyote ili aendelee kutetea wanyonge ambao wameporwa haki yao, kikubwa kinachotakiwa ni kutenda haki kwa kila anayestahili pasipokumwonea yeyote.

# Tatoa yaomba Serikali Tanzania, Kenya kutatua kero mpakani

**Na Mary Geofrey**

CHAMA cha Wamiliki wa Malori (Tatoa), kimeiomba serikali kutatua changamoto nne zinazojitokeza katika mipaka ya nchi za Kenya na Rwanda zinazosababisha kukwamisha shughuli za kiuchumi nchini.

Kimetaja changamoto hizo kuwa ni unyanyasaji na unyanyapaa wa madereva wa Tanzania, kutokuwapo kwa usawa wa ufanyaji wa biashara, gharama za ufanyaji biashara na vyeti vya Covid-19 vinavyotolewa kwa madereva.

Makamu Mwenyekiti wa Tatoa, Elias Lukumay, alieleza hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari.

"Tatoa inaomba serikali kuingilia kati jambo hili kwa undani na kuomba kurejea kwenye meza ya mazungumzo na nchi jirani ili changamoto hizo zipatiwe ufumbuzi wa haraka.

Alisema wanapendekeza vyeti vya Covid-19 vinavyotolewa na Wizara ya Afya vitambulike na kutumika bila kikwazo.

Akielezea changamoto hizo alisema madereva wa Tanzania wanakumbana na unyanyasaji katika mpaka wa Rwanda na Namanga, nchini Kenya na kwamba wapo waliokaa muda mrefu mpaka wa Rusumo wakisubiri kushusha mizigo na wengine wakisubiri kuvuka kuelekea nchini Congo.

"Madereva hawa wamekuwapo katika eneo ambalo halina huduma toshelezi za kijamii kwa idadi kubwa wakisubiri kuvuka na hata wale waliovuka kuingia Rwanda kwa utaratibu uliowekwa wa kusindikizwa bado wanapitia mazingira magumu ya kukosa huduma za kijamii," alisema Lukumay. Kadhalika, alisema utaratibu uliopo kwa sasa, magari ya Tanzania yanatakiwa kuishia mpakani isipokuwa kwa yanayobeba mizigo iliyoainishwa kama bidhaa muhimu, wakati huo huo, magari ya Rwanda yanaruhusiwa kusafiri zaidi ya kilometa 1,000 kwenda Dar es Salaam kuchukua mizigo.

"Utaratibu huu umesababisha waagizaji wa mizigo kupendelea zaidi kutumia magari ya Rwanda kwa sababu yanawapelekea mizigo hadi mlangoni wakati magari ya Tanzania yanaishia mpakani hivyo kufanya mazingira ya biashara kutokuwa sawa kwa pande mbili," alisema Lukumay.

Kuhusu changamoto ya tatu alisema gharama za ufanyaji biashara zimeongezeka kwa sababu eneo lililotengwa na Serikali ya Rwanda ili kushusha mizigo, miundombinu hafifu ya ushushaji, uhudumiaji na uhifadhi wa mizigo, hivyo kusababisha magari ya Tanzania kukaa muda mrefu mpakani wakati magari ya Rwanda yakifaulisha mizigo.

"Ucheleweshaji huu unasababisha wasafirishaji wa Tanzania kuendelea kutozwa faini za kontena ya hadi Sh. 120,000 kwa siku kwa kontena moja kwa kuchelewesha kurudisha kontena tupu kwa wenye meli," alisema Lukumay.

Kuhusu vyeti vya Covid-19 vinavyotolewa kwa madereva, alisema makubaliano yaliyofikiwa Kenya hivi karibuni, ilikuwa ni madereva kupima na kupata cheti ambacho kingekubalika pande zote na kumwezesha dereva kuvuka bila vikwazo.

Alisema pamoja na makubaliano hayo mamlaka za Kenya zimebadilika ghafla na kuvikataa vyeti hivyo bila kutoa taarifa, hali iliyosababisha madereva kuendelea kupata tabu katika mpaka wa Namanga na kusababisha hasara kwa wafanyabiashara hasa waliosafirisha bidhaa zinazoharibika kwa haraka.

Vile vile, alisema Tatoa inatambua mchango mkubwa wa madereva kwa sababu wamekuwa mastari wa mbele katikati ya mapambano ya janga la Covid-19 kwa kujituma na kuhakikisha vifaa muhimu vya kuokoa maisha kama dawa, PPE na vifaa vingine muhimu vinawafikia watu wa nchi jirani.



Ofisa Mauzo wa kampuni ya Bia Tanzania (TBL), Catherine Lyakurwa (wa pili kushoto), akimkabidhi moja ya mfuko wenye vifaa vya kujikinga na ugonjwa wa corona, vilivyotolewa na kampuni hiyo kwa Meneja wa baa ya Africana, Andrew Kessy, kwa ajili ya kuwakinga wahudumu na wateja jijini Arusha. **PICHA: MPIGAPICHA WETUi**

# Hukumu kesi ya anayedaiwa kubaka mtoto yawekwa kiporo

**Na Mwandishi Wetu,**

**PEMBA**

KESI ya kutorosha na kubaka inayomkabili mtuhumiwa Abdul-rahman Ubwa Daudi (Tumbo Joto), mkazi wa Selemu Wete, imeahirishwa kutokana na hakimu anayeshughulikia kesi hiyo kwenda likizo.

Kesi hiyo iliahirishwa na Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo, Maulid Ali Hamad, hadi Juni 18, mwaka huu kwa ajili ya kutolewa hukumu.

"Mheshimiwa hakimu, shauri hilo lipo kwa ajili ya hukumu ingawa hakimu anaeshughulikia kesi hiyo yuko likizo, hivyo tunaiomba mahakama yako kulipangia tarehe nyengine kwa ajili ya hukumu", alisema mwendesha mashtaka kutoka Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), Ali Amour Makame.

Hakimu Maulid hakuwa na pingamizi, na kusema ni vyema shauri hilo likarudi tena Juni 18, mwaka huu.

Awali ilidaiwa mtuhumiwa huyo alitenda makosa mawili ambapo kosa la kwanza alilitenda Oktoba 18, mwaka 2019, kwamba bila ya halali na bila yaridhaa ya wazazi wake alimtorosha mtoto wa miaka 17 kutoka nyumbani kwao Chasasa na kumpeleka Bopwe.

Kosa la pili, ilidaiwa mtuhumiwa huyo alilitenda siku hiyo hiyo majira ya saa 06:00 mchana katika eneo la Bopwe Wilaya ya Wete, Mkoa wa kaskazini Pemba, alimbaka mtoto wa kike mwenye umri wa miaka17 mkaazi wa Chasasa shehia ya Utaani.

Kufanya hivyo ni kosa kisheria kinyume na kifungu cha 108 (1) (2) (e) na 109 (1) cha Sheria ya adhabu namba 6 ya mwaka 2018 sheria ya Zanzibar.

# Programu P4R yaokoa bil. 8.4/-

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

KUPITIA programu ya Lipa kwa Matokeo (P4R), Wakala wa Usambazaji wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (Ruwasa), imeokoa Sh. bilioni 8.4 kwa kununua vifaa kwa pamoja ngazi ya taifa.

Hayo yalibainishwa na jana na Mkurugenzi Mkuu wa Ruwasa, Clement Kivegalo, katika hafla ya utiliaji saini wa mikataba kwa washindi wa zabuni 11 zilizotangazwa na wakala huo.

Alisema asilimia 70 ya gharama za miradi ya maji huenda kwenye mabomba na hivyo kufanya mchakato wa ununuzi wa mabomba na pampu katika ngazi ya kitaifa ya Ruwasa.

"Ili kuepukana na ucheleweshwaji wa miradi iliyotokana na kutokuwapo kwa bodi za zabuni tuliamua kufanya manunuzi ya pamoja kwenye vifaa," alisema.

Alisema vifaa kama nondo, saruji, mbao na mchanga walifanya katika ngazi ya mkoa.

Alitaja sababu za kufanya hivyo ni kuharakisha mchakato wa ununuzi wa vifaa hivyo, kusimamia kwa karibu ubora wa vifaa.

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, aliagiza Ruwasa kuzitengenezea miradi mingine fedha ambazo wameziokoa kutokana na programu hiyo ili kupata huduma ya maji.

"Miaka ya nyuma niliwahi kuhoji inakuaje serikali ikawa na mkandarasi wa kununua mabomba kwa kuwa hawavijui viwanda, leo hii hawa watu wa viwanda husika wamekuja hapa na tumeweza kusainiana nao na tunajivunia tumeokoa zaidi ya Sh. bilioni nane," alisema.

Awali, Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Prof. Kitila Mkumbo, alisema programu ya P4R inatekelezwa katika mikoa 17 nchini na serikali imekopa Sh. bilioni 800.

"Kwa mwaka 2019/20 Ruwasa imetekeleza miradi 513 ambayo itazalisha vituo vya kuchotea maji 9,286 kwenye mikoa hiyo 17, hii ni programu ya miaka mitano, huu ni mwaka wa kwanza," alisema.


**CHAMA CHA WAFANYAKAZI WA SERIKALI ZA MITAA TANZANIA (TALGWU)**

**TANGAZO LA NAFASI ZA AJIRA**

Katibu Mkuu wa Chama cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa (TALGWU) anawatangazia nafasi ya Ajira kama ifuatavyo:-

**1.0 AFISA TEHAMA DARAJA LA I TLGS D (Nafasi 1)**

**1.1 SIFA NA UZOEFU**

(i) Kuajiriwa mwenye shahada ya kwanza au Stashahada ya juu ya Kompyuta katika moja ya fani zifuatazo; Sayansi ya Kompyuta, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Menejimenti ya Mifumo ya Habari au mafunzo mengine yanayohusiana na fani hii.
(ii) Awe na uzoefu wa kufanya kazi si chini ya miaka mitatu (3)
(iii) Awe na Ufahamu zaidi wa mifumo ya kutunza Takwimu (Data Base)
(iv) Awe na umri usiozidi miaka 45.

**1.2 KAZI ZA KUFANYA**

(i) Kutunza na kuhakiki mfumo wa hifadhi Data
(ii) Kutoa huduma za hifadhi Data kwa watumiaji.
(iii) Kutengeneza kiunganishi kati ya hifadhi Data na Programu tumizi (Develop back – end and front – end connectivity)
(iv) Kusanifu, kutengeneza na kufanya majaribio ya Programu za hifadhi – Data (Design, Implement and test Data Base)
(v) Kuweka usalama wa hifadhi Data ( Implement Security and access control into database)
(vi) Kufanya majaribio ya vifaa vya mtandao wa kompyuta (Test network equipment and devices)
(vii) Kusimamia utekelezaji wa maelekezo ya usalama wa mtandao kwa mujibu wa miongozi ya usalama wa mtandao wa kompyuta, (Implement network security guide lines)
(viii) Kufanya kazi nyingine atakazo pangiwa na Mkuu wake wa Kazi zinazoendana na sifa na fani yake.

**3.0 NAMNA YA KUTUMA MAOMBI**

Waombaji wenye sifa zilizotajwa watume maombi yao kwa:-

**Katibu Mkuu,**
**Chama cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa (TALGWU),**
**S. L. P. 16097,**
**DAR ES SALAAM.**

**NB.** Barua zote za Maombi ni lazima ziambatanishwe na Wasifu (CV) wa muombaji, picha moja ya Passport size ya hivi karibuni. Na nakala zilizothibitishwa za viwango vya ufaulu na vyeti vya taaluma. Majina matatu ya Wadhamini yaonyeshe anuani na namba zao za simu. Maombi yatumwe kwa njia ya posta.

Pia Tangazo hili linapatikana kwenye Tovuti ya TALGWU www.talgwu.or.tz.

Mwisho wa kutuma maombi ni siku kumi na nne (14) tangu tarehe ya tangazo hili.

**Rashid M. Mtima,**
**KATIBU MKUU – TALGWU.**

215767102

# Waziri: Majadiliano na Kenya yanaendelea

**Na Enock Charles**

SERIKALI imesema ipo katika majadiliano na viongozi wa Kenya ili kutatua tatizo la kutotambuliwa kwa matokeo ya vipimo vya ugonjwa wa corona wanavyopima madereva wa malori wanapovuka mpakani.

Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Dk. Damas Ndumbaro, aliyasema hayo jana alipotembelea Chuo cha Diplomasia jijini Dar es Salaam jana.

Dk. Ndumbaro alisema kuna baadhi ya viongozi kutoka Kenya ambao wamekuwa hawavitambui vipimo kutoka Tanzania, jambo ambalo amesema serikali inalitafutia ufumbuzi wa haraka.

"Tulikaa tukakubaliana kuwa maamuzi yaliyotolewa na Mawaziri wa Afrika Mashariki na Mawaziri wa Afya yaheshimiwe na yatekelezwe na tukaanza kutekeleza," alisema Dk. Ndumbaro.

Alisema lengo la serikali ni kuimarisha ushirikiano wa kibiashara na kuzisaidia nchi jirani ambazo hazina bandari kufanya biashara kupitia bandari za hapa nchini.

Akiongea na wanafunzi wa chuo hicho ambao walimuuliza maswali mbalimbali na kuzungumzia suala la ajira, Dk. Ndumbaro aliwataka wanafunzi hao kutokuitegemea serikali katika kuwapa ajira kwa kuwa haiwezi kuajiri wanafunzi wote watakaohitimu mafunzo katika chuo hicho.

"Serikali ina mwisho wake katika kuajiri kama wanahitajika watu sita mahali huwezi kuweka 10," alisema Dk. Ndumbaro.

Aidha, aliwataka wanafunzi hao na waliohitimu katika chuo hicho kutokata tamaa katika kuomba ajira katika Jumuiya za Kimataifa kama vile Umoja wa Mataifa (UN), Umoja wa Afrika (AU) na jumuiya nyingine mbalimbali za ushirikiano wa mataifa.



Raia wa Armenia, Vardan Mkhitaryan akiwa chini ya ulinzi wa askari polisi katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Raia Armenia kortini madai uhujumu uchumi

**Na Hellen Mwango**

RAIA wa Armenia, Vardan Mkhitaryan (47) na mlinzi Rosemary Mwemezi (32), wamefikishwa mahakamani wakikabiliwa kesi ya uhujumu uchumi.

Pia wanadaiwa kula njama, kufanya udanganyifu kwenye vifaa vya mawasiliano na kuisababishia serikali hasara ya Sh. milioni 44.5.

Washtakiwa hao walisomewa mashtaka yao katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Agustina Mmbando.

Wakili wa Serikali Jaqline Nyantori alidai kati ya Oktoba Mosi, 2019 na Mei 28, mwaka huu mahali pasipofahamika jijini Dar es Salaam, washtakiwa walikula njama ya kutenda kosa la kufanya mawasiliano kwa njia ya udanganyifu.

Shtaka la pili, ilidaiwa kati ya Oktoba Mosi na 30, 2019 jijini Dar es Salaam, Mkhitaryan aliingiza nchini mitambo ya mawasiliano bila kibali cha Mamlaka ya Mawasiliano ya Tanzania (TCRA).

Shtaka la tatu, ilidaiwa kati ya Oktoba Mosi na 30, 2019 eneo la Mbezi Beach, Wilaya ya Kinondoni isivyo halali, Mkhitaryan alifunga mitambo ya mawasiliano ya masafa ya nje ya nchi kupitia kadi ya Airtel bila leseni ya TCRA.

Nyantori alidai katika shtaka la nne, kati ya Oktoba 10,2019 na Mei 28, 2020 eneo la Mbezi Beach Wilaya ya Kinondoni, jijini Dar es Salaam, Mkhitaryan alifunga mitambo ya mawasiliano ya simu za kimataifa bila leseni ya TCRA.

Jamhuri uliendelea kudai katika shtaka la tano, kati ya Oktoba 10, 2019 eneo la Mbezi washtakiwa wote wawili kwa nia ya kukwepa kulipa kodi ya kipato stahiki walitoa mawasiliano ya simu za kimataifa bila kuwa na leseni ya TCRA.

Katika shtaka la sita, ilidaiwa kati ya Oktoba 10, 2019 na Mei 28, mwaka huu eneo la Mbezi Beach Wilaya ya Kinondoni jijini Dar es Salaam, Mkhitaryan alitumia mitambo ya mawasiliano bila kuthibitishwa na TCRA.

Katika shtaka la saba, ilidaiwa kati ya Oktoba 10, 2019 na Mei 28, mwaka huu eneo la Mbezi Beach, Wilaya ya Kinondoni, , washtakiwa wote wawili waliisababishia TCRA hasara ya Washtakiwa hawakutakiwa kujibu chochote kwa sababu mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi za uhujumu uchumi mpaka Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) atakapotoa kibali.

Nyantori alidai upelelezi wa kesi hiyo haujakamilika, hivyo

Hakimu Mmbando alisema kesi hiyo itatajwa Juni 18, mwaka huu, na washtakiwa wapelekwe mahabusu.

# Dodoma kutobadilishwa kuwa makao makuu

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

BUNGE la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, jana lilipitisha azimio la serikali kutobadili uamuzi wa Jiji la Dodoma kuwa makao makuu ya nchi na shughuli za serikali.

Akiwasilisha hoja hiyo, Stanslaus Mabula, Mbunge wa Nyamagana (CCM), alisema Bunge linaazimia kuitaka serikali, mamlaka au mtu yeyote kutotengua uamuzi wa wananchi wa kuifanya Dodoma kuwa makao makuu ya nchi na kuitaka serikali na taasisi zake kutohamisha kwa namna yoyote shughuli za serikali kutoka Dodoma kwenda sehemu nyingine yoyote ya nchi.

Alisema Bunge pia linaazimia kuitaka serikali kuhakikisha kwamba inaendelea kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kuboresha na kuendeleza miundombinu ya Jiji la Dodoma wakati wote, ili kulifanya kuwa na mandhari inayoendana na hadhi ya makao makuu ya nchi na serikali.

# Vijana Chadema waitwa kuwania uchaguzi mkuu

**Na Elizabeth Zaya**

NAIBU Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) Zanzibar, Salum Mwalimu, amewashauri vijana wa chama hicho kujitokeza kwa wingi kugombea nafasi mbalimbali za uongozi kupitia chama hicho, katika uchaguzi mkuu.

Alitoa ushauri huo alipofungua kikao cha Kamati ya Utendaji ya Baraza la Vijana la chama hicho (Bavicha), kilichofanya mkutano wake kwa njia ya kidijitali jana.

Alisema katika kipindi hiki cha uchaguzi ni vyema vijana wakajitokeza kugombea nafasi mbalimbali bila kutakatishana tamaa na kuwataka kuhakikisha wanayojadili yanaleta masilahi kwa chama chao.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Bavicha Taifa, John Pambalu, alisema katika kuelekea uchaguzi huo, ni vyema vijana wakatiana moyo wenyewe kwa wenyewe ili wajitokeze kwa wingi kuwania nafasi mbalimbali za uongozi.

"Tusiwe sehemu ya kuwaumiza na kuwakatisha tamaa vijana na wanachama wetu wanaotaka kuwania nafasi mbalimbali za uongozi, tutiane moyo wenyewe kwa wenyewe," alisema Pambalu.

# CCM Iringa yaonya walioanza kampeni

**Na Francis Godwin,** IRINGA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM ) Mkoa wa Iringa kimetoa onyo kwa wanachama wake, ambao wameanza kampeni za chini kwa chini kwa ajili ya ubunge na udiwani.

Imesema kuwa taarifa zao zinajulikana na wajiandae kisaikolojia kuona majina yao yanakatwa watakapojitokeza kuchukua fomu za kuwania nafasi hizo.

Katibu wa CCM Mkoa wa Iringa, Dk. Abel Nyamahanga, alitoa onyo hilo wakati wa kikao cha Baraza Kuu la Jumuiya wa Wanawake wa CCM (CWT) kuwa ndani ya CCM kuna utaratibu wa kufanya kampeni na kutangaza nia, na kuwa wote ambao wametangaza nia sasa ama kuanza kampeni huku wakijua muda wa kufanya hivyo bado, wanavunja kanuni za chama na wajiandae kuwajibishwa.

Alisema chama kimeweka watu wake maalum kwenye kata na majimbo yote kuorodhesha majina ya wanaojipitisha kushawishi wanachama kuwapigia kampeni za nafasi wanazotaka kugombea huku wakijua kufanya hivyo ni kuvuruga taratibu za chama.

"Wapo ambao wanataka udiwani na ubunge wa viti maalum na ubunge wa majimbo na wamekuwa wakipita pita huku mitaani kushawishi wanachama... nasema wote wanaofanya hivyo tunawajua na majina yao tunayo na watambue kuwa wanapita kwa hila, adhabu ya watu hao inachemka na wakati wa kuchukua fomu watapewa adhabu yao," alisema Dk. Nyamahanga.

Alisema kutangaza nia kufikiri kugombea baada ya Bunge kuvunjwa sio dhambi, ila dhambi ni kuanza kupita kwenye majimbo kushawishi wanachama na kutoa rushwa kwa lengo la kuwaaminisha wanachama kuwa mhusika ni bora na kuliko wengine, jambo ambalo linavuruga chama na kutengeneza makundi.




Meneja Biashara wa Kampuni ya Yara, Kanda ya Kaskazini, Phillipo Mwakipesile (kushoto), akikabidhi vifaa saidizi vya kupambana na janga la Covid-19 kwa mmoja wa mawakala wa kampuni hiyo, Mzee Ngoyi (kulia). Wakishuhudia kutoka kulia ni Katibu Tawala Msaidizi wa Mkoa wa Arusha-Utawala, David Lyamongi na Mganga Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Wedson Sichalwe. Kampuni hiyo ilikabidhi msaada huo kwa mawakala wake na wakulima. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Wadau walivyojadili kilimo cha pamba

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

WAKULIMA nchini watakiwa kulima kilimo cha kisasa ili kuongeza uzalishaji wenye tija, kujikita katika kilimo cha biashara na kuondokana na kilimo cha kujikimu.

Hayo yamebainishwa na Waziri wa Kilimo, Japhet Hasungwa, wakati wa mkutano wa Bodi ya Pamba Tanzania mkoani Mwanza na kuwakutanisha wadau wa tasnia ya pamba na wadau kutoka serikalini.

Hasunga alisema, wakulima wanapaswa kuhamasishwa kwenye kilimo cha kisasa ili kuongeza uzalishaji kwa kutumia pembejeo bora na teknolojia ya kisasa, ambayo mkulima ataweza kupata kilo 1,350 kwa hekari moja kama nchi nyingine zinazolima pamba.

Alisema wengi kwa sasa wanapata kilo 150,200, hivyo alisema ifike mahali wafuate maelekezo na kuzingatia kanuni za kilimo cha kisasa, na dhamira ya serikali ni kuhakikisha kuwa kilimo nchini kinakuwa cha kibiashara na kuondokana na kilimo cha kujikimu.

Pia anasema, ifike mahali zao la pamba yote nchini inachakatwa ndani ya nchi kwa kuhakikisha viwanda vinafufuliwa na watu wanawekeza ili kuwe na uhakika wa soko.

"Asilimia 65 ya viwanda inategemea malighafi kutoka kwenye kilimo hivyo lazima tuwezeshe mfumo wa kilimo wa kisasa, kwani kilimo ndio kinatupatia asilimia 100 ya chakula." alisema.

Naibu Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Dk. Bernard Kibese, alisema hali ya uchumi ipo vizuri haijateteleka licha ya uwapo wa corona, huku akiwahakikishia wakulima wa pamba kuwa soko lipo kwani vyombo vya fedha vipo tayari kununua pamba yote itayazozalishwa nchini, na kuwa hakuna mnunuzi atakaye kosa mkopo.

"Tuache kumpa hela mkulima za manunuzi ya pamba, naagiza benki zote hakuna mkulima yeyote atakayepewa fedha mkononi isipokuwa kupitia akaunti za benki, hivyo kwa mkulima ambaye hana akaunti akafungue akaunti," alisema Naibu Gavana.

Naye Mwenyekiti wa kamati ndogo ya wadau wa pamba ambaye ni Mkuu wa Mkoa wa Mara, Adam Malima, alisema nchi inatakiwa kuwa na uzalishaji wenye tija, na kuwa huku lengo ni ifikapo mwaka 2020/23 iwe imezalisha tani milioni moja za pamba.

Naye Mwenyekiti wa wanunuzi wa pamba, Christopher Gachuma, alisema hatujawahi kuona mkutano mzuri wakati huu ni wa kufanya kazi kwa pamoja pasipo mvurugano ili kuboresha na kuinua sekta hiyo katika soko la dunia na kuondokana na dhana ya kuwa pamba ya Tanzania ni chafu.

## Mapendekezo mazingira biashara kufanyiwa kazi

**Na Enock Charles**

BARAZA la Taifa la Biashara (TNBC) limepokea ripoti iliyoandaliwa na Taasisi ya Utafiti ya Repoa kwa kushirikiana na Sweden, Denmark, Norway na Finland inayoeleza hali ya uwekezaji na mazingira ya biashara kwa nchi hizo nchini, na kuahidi kuyafanyia kazi mapendekezo yaliyomo.

Akizungumza wakati wa makabidhiano ya ripoti hiyo jijini Dar es Salaam, Katibu Mtendaji wa TNBC, Dk. Godwill Wanga, alisema tafiti zenye weledi zinazoelezea hali ya mazingira ya biashara na uwekezaji zinachangia kwa kiasi kikubwa katika kutatua changamoto zilizopo na kuweka mazingira mazuri zaidi ya kibiashara.

"Tumepokea ripoti kutoka Repoa ambayo inaeleza namna serikali ilivyofanikiwa kuweka mazingira rafiki na kuwezesha biashara na uwekezaji pamoja na kutaja maeneo ambayo bado changamoto," alisema na kuongeza kuwa serikali imedhamiria kuhakikisha mazingira ya biashara yanaendelea kuimarika na kuvutia wawekezaji zaidi.

Dk. Wanga alisema licha ya jitihada kubwa zilizochukuliwa na serikali katika kuweka mazingira rafiki ya ufanyaji biashara Tanzania,

## ActionAid yasaidia vifaa vya corona

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

SHIRIKA lisilo la Kiserikali la ActionAid Tanzania limekabidhi vifaa vya kunawia mikono kwa ajili ya kujikinga na maradhi ya corona kwa uongozi wa Hospitali ya Wete pamoja Shule ya Sekondari Utaani.

Akikabidhi vifaa hivyo kwa Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Katibu Tawala Wilaya ya Wete, Mkufu Faki Ali, alisema ActionAid imekuwa mstari wa mbele kusaidia jamii katika nyanja mbalimbali.

Alieleza utaratibu huo ambao wamejipangia taasisi hiyo ni jambo zuri, hivyo aliiomba kuendelea kusaidia pale panapohitajika kufanya hivyo.

Mkufu aliwatahadharisha wananchi wa Wilaya ya Wete kuwa bado ugonjwa wa corona upo, hivyo waendelee kuchukua tahadhari na kujikinga.

Katibu huyo alisema licha ya serikali kujitahidi kutoa elimu juu ya kujikinga na ugonjwa huo, lakini bado kuna baadhi ya wananchi wanabeza juhudi hizo na kukaidi maelekezo yote yanayotolewa na wataalamu.

"Kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya ya Wete ninawaambia wananchi wote kuwa waache tabia hii na waendelee kuchukua ya kujikinga na ugonjwa wa corona," alisema Mkufu.

Aliwataka wazazi na walezi wa wanafunzi wanaosoma katika shule hiyo wa kidato cha sita kuwaruhusu watoto wao, ili waendelee na masomo pamoja na kujianda kwa mitihani ambayo inatarajiwa kufanyika mwishoni mwa mwezi huu.

HABARI BUNGENI

# Serikali yafunguka ajira walimu masomo ya sanaa

SERIKALI imesema itaajiri walimu wa masomo ya sanaa pale idadi ya walimu wa masomo ya sayansi, hisabati, kilimo, biashara, elimu maalum na mafundi sanifu wa maabara za shule katika shule za sekondari itakapori-dhisha.

Aidha, imesema wakati ikiendelea na mchakato wa kujaza nafasi za walimu wa sayansi, wahitimu wa kada ya ualimu wa masomo ya sanaa wanahimizwa kutafuta ajira katika taasisi nyingine za umma na shule binafsi.



Hayo yalielezwa jana bungeni na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora katika swali la Mbunge wa Korogwe Mjini (CCM), Mary Chatanda.

Katika swali lake Mbunge huyo, alisema wahitimu wa kada ya walimu wa masomo ya sanaa ngazi ya stashahada na shahada kuanzia mwaka 2015 hadi leo hawajapata ajira.

"Je, nini hatima ya walimu wa kada hizi?" Alihoji.

Katika majibu ya ofisi hiyo, ilisema katika utumishi wa umma, nafasi za ajira za watumishi wa kada mbalimbali wakiwamo walimu hutengwa kulingana na vipaumbele vya serikali.

Ilisema katika miaka ya nyuma ambapo watumishi wa umma wenye sifa walikuwa wachache, serikali ilitoa ajira za moja kwa moja kutoka vyuoni kwa kada zote.

"Kutokana na kuwa na watumishi wa kutosha na ili kupata watumishi wenye sifa, weledi na uadilifu, serikali ilibadilisha utaratibu wa ajira za moja kwa moja na kuanza kutoa ajira kwa njia ya ushindani kupitia usaili wa watumishi wa kada mbalimbali isipokuwa walimu na watumishi wa kada za afya," ilisema.

Ilieleza kuwa katika miaka ya hivi karibuni, utumishi wa umma umekabiliwa na changamoto kadhaa ikiwa ni pamoja na kukosekana kwa baadhi ya kada katika soko la ajira hususani kwa baadhi ya kada za Afya na Elimu (Masomo ya Sayansi).

"Kutokana na changamoto hii, serikali imeweka kipaumbele cha ajira mpya kwa walimu wa masomo ya Sayansi, Hisabati, Kilimo, Biashara na Elimu Maalum pamoja na fani ya Fundi Sanifu wa Maabara za Shule," ilisema.

Hata hivyo, ilisema kutokana na kuwapo kwa walimu ziada wa masomo ya sanaa katika shule za sekondari hususan katika maeneo ya mijini, serikali iliwaagiza waajiri katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kufanya tathmini ya mahitaji halisi ya walimu.

Pia alisema kuhamishia walimu wa ziada katika shule za msingi na maeneo yenye upungufu mkubwa wa walimu ili kuweka uwiano mzuri wa walimu kwa wanafunzi.

"Ninapenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa serikali itaajiri walimu wa masomo ya sanaa pale idadi ya walimu wa masomo ya sayansi, hisabati, kilimo, biashara, elimu maalum na mafundi sanifu wa maabara ya shule katika shule za sekondari itakapori-dhisha," ilisema.

# Tanzania sasa ina balozi 43 duniani






Habari na Augusta Njoji

BUNGE limeelezwa kuwa hadi sasa, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ina balozi 43 kwenye nchi mbalimbali duniani.

Hayo yalibainishwa jana bungeni na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ilipokuwa ikijibu swali la Mbunge wa Malindi (CUF), Ally Saleh Ally.

Katika swali lake, mbunge huyo alisema dunia inayokua kwa mfungamano na uhusiano wa kiuchumi na kidiplomasia, ni wazi kuwa suala la kufungua balozi mpya huwa lazima kadri ya hali inavyohitaji.

"Je, ni taratibu gani zinatumika kufanya maamuzi ya idadi ya balozi duniani kwa wakati mmoja, je, mgawanyiko wa balozi kwa kila bara hufanywa kwa misingi ipi?" Alihoji.

Pia alihoji kama kuna dira inayoonyesha mipango ya ufunguzi wa balozi mpya.

Katika majibu ya wizara hiyo, ilisema utaratibu wa nchi kufungua ubalozi katika nchi fulani hutegemeana na maslahi ya Taifa katika masuala ya kisiasa, kiuchumi, kidiplomasia, kijamii, kiulinzi na mengineyo.

"Pamoja na maslahi hayo pia uwezo wa nchi kifedha ndiyo huongoza nchi yetu kufungua balozi katika nchi/ukanda upi na kwa wakati gani," ilisema.

Hata hivyo, ilisema hadi sasa, serikali ina balozi 43 na Balozi nane kati ya hizo (Qatar, Cuba, Jamhuri ya Korea, Israel, Algeria, Namibia, Sudan na Uturuki) zimefunguliwa katika kipindi cha serikali ya awamu ya tano.

Aidha, ilisema serikali inaendelea kufanya tathmini mbalimbali kila mara ili kubainisha maeneo au nchi ambazo inahitaji kufungua ubalozi kwa kuzingatia mabadiliko ya kiuchumi, kisiasa na kijamii yanayotokea ndani na nje ya nchi.



# Kibano watendaji ushirika kuendelea

WIZARA ya Kilimo kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika, imesema itaendelea kuwabana viongozi na watendaji wa vyama vya ushirika kwa kutoa adhabu kali kwa wahusika wa ubadhirifu wa fedha na mali za umma.

Aidha, ukaguzi wa Vyama vya Ushirika nchini (AMCOS) katika Mkoa wa Mara umebaini ubadhirifu wa Sh. milioni 47.1 za wakulima.

Kauli hiyo ilitolewa jana bungeni na wizara hiyo ilipokuwa ikijibu swali la Mbunge wa Bunda Vijijini (CCM), Boniphace Mwita.

Katika swali lake mbunge huyo, alisema lengo la kuanzisha AMCOS lilikuwa kuwakusanya pamoja wakulima na kuwa na nguvu ya kusimamia malipo mazuri toka kwa wanunuzi.

"Lengo hili limekuwa kinyume na matarajio ya wakulima ambapo wahusika wa AMCOS nyingi wamekuwa wezi wa fedha za wakulima kwa kutowalipa na kuwaibia kupitia upimaji wa kilo hususan kwenye pamba," alisema.

Alihoji serikali ina mkakati gani wa kutatua tatizo hilo kwa wakulima wa pamba nchini.

Katika majibu ya wizara hiyo, ilisema sambamba na kuwabana viongozi pia itatoa mafunzo rejea mara kwa mara ili watekeleze majukumu yao kwa ufanisi.

Ilisema serikali imeendelea kusimamia vyama hivyo kwa kufuata kanuni na taratibu kwa mujibu wa Sheria ya Ushirika Namba 6 ya Mwaka 2013 kwa lengo la kuimarisha ufanisi na kupunguza dosari mbalimbali za kiutendaji ikiwa ni pamoja na wizi na matumizi mabaya ya fedha za wakulima.

Ilisema Mkoa wa Mara una AMCOS 559, kati ya vyama hivyo 133 sawa na asilimia 23.8 vimekaguliwa.

"Ukaguzi uliofanywa kwenye vyama hivyo vya mazao (AMCOS) katika mkoa huo umebaini dosari kadhaa katika vyama hivyo ikiwamo uandishi mbovu wa vitabu, ubadhirifu wa fedha wa jumla ya Sh. milioni 47.1 na hivyo wakulima 103 kutokulipwa stahili zao," ilisema.

Kwa upande wa Wilaya ya Bunda, ilisema zipo AMCOS 119 ambapo 21 sawa na asilimia 17.65 zimekaguliwa.

Aidha, ilisema Wilaya ya Bunda Vijijini kumebainika upungufu wa fedha kiasi cha Sh. milioni 45 na kesi tatu zipo mahakamani ili wote watakaobainika kuhusika wachukuliwe hatua stahiki.

"Kuhusu kuibiwa kwa wakulima kupitia mizani, serikali kupitia wakala wa vipimo hufanya ukaguzi kila mwaka kabla ya msimu kuanza ili kuhakiki ubora wa mizani hizo," ilisema.

Kadhalika, ilisema Tume ya Maendeleo ya Ushirika na Bodi ya Pamba Tanzania wanaendelea kuhakikisha kwamba mizani zinazotumika zimehakikiwa na kuwekewa alama maalum ili kuzuia kuchezewa kwa lengo la kumwibia mkulima.

"Aidha, serikali imeelekeza kampuni zinazonunua pamba kuwalipa wakulima fedha za mauzo ya pamba kupitia akaunti zao za benki na sio kupitia AMCOS," ilisema.

Nipashe
# TESA
Jumanne Juni 9, 2020
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 14

**Simujanja ilivyommaliza ofisa wa polisi Marekani**



Ukurasa 13

Motisha yaichomoa shule toka mkiani hadi 10 bora



Ukurasa 12

**Ni mlolongo wa faida mtoto, wazazi, taifa**

ELIMU

## MASOMO YANAPOANZA...

# La muhimu kujali muda, tahadhari, kutokomoana

**NA REUBENI LUMBAGALA**

KUOKOA muda, kuchukua tahadhari na umakini zaidi kwenye kufundisha na kusoma ni suala la msingi wakati huu shule na vyuo vinapoanza tena masomo baada ya likizo ya corona.

COVID -19 ilisababisha taasisi za elimu kuanzia shule za msingi hadi vyuo vya kati na vikuu kufungwa kuanzia Machi 17mwaka huu.

Ni kufuatia agizo la serikali lililotolewa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, ili kuzuia usambaaji wa maradhi hayo.




Mabango yenye ujumbe mahususi ni mojawapo ya njia zinazotumiwa vyuo vikuu kuhimiza tahadhari na kujikinga na corona:**PICHA: MTANDAO**

Kutokana na ahueni iliyopatikana kwa sasa, serikali imeruhusu wanafunzi wa kidato cha sita, vyuo vya kati na vikuu kurejea masomoni kuanzia mwanzoni mwa mwezi huu (Juni 1).

Licha ya kuendelea na masomo msisitizo ni wanafunzi na walimu wao kuendelea kuchukua tahadhari na kufuata ushauri na miongozo yote inayotolewa na wataalam wa Wizara ya Afya ili kuendelea kuwa salama zaidi.

Sekta ya elimu ni miongoni mwa maeneo ambayo yameathirika moja kwa moja kutokana na janga la corona ndiyo maana shule na vyuo vilifungwa kwa kwa zaidi ya miezi miwili.

Mihula ya masomo inabadilika kutokana na wanafunzi kurudi nyumbani kwani walipaswa kuwa shuleni wakiendelea na masomo lakini walilazimika kuwa likizoni. Katika kipindi cha likizo ya corona, baadhi ya shule na vyuo vimeweka mikakati ya kufidia muda uliopotea ili wanafunzi wapate maarifa, ujuzi na stadi kama ilivyotarajiwa ili wawe wahitimu bora.

Kikubwa ni wakufunzi na wahadhiri kuhakikisha kuwa pamoja na nia njema waliyonayo ya kufidia muda uliopotea kufuatia likizo ya corona, ni lazima pawapo na umakini mkubwa wa utekelezaji wa mikakati yao ili wanafunzi wapate maarifa stahiki.

Ni wazi kuwa kama watatekeleza mikakati hiyo kwa kasi kubwa bila kuzingatia ubora, wanafunzi watashindwa kuelewa kile watakachofundishwa na hatimaye kukwama kufikia malengo.

Wanafunzi wa kidato cha sita na wale wa vyuo vya ualimu wana majuma manne (mwezi mmoja), kuanzia pale walipofungua hadi kuingia kwenye mtihani wa taifa wa kidato cha sita (ACSEE) na ile ya kuhitimu mafunzo ya ualimu. Walimu wanapaswa kuendelea kuwafundisha wanafunzi huku wakifanya marudio ya kutosha ili kuwaandaa vyema wanafunzi wao kumudu mitihani yakitaifa, ili kusonga mbele kimasomo.

Mikakati iliyowekwa na uongozi wa shule na vyuo iwe chachu ya kuwasaidia wanafunzi kufanya vyema badala ya kugeuka mateso kwao.

Kwa wakufunzi na wahadhiri wa vyuo vikuu waendelee na utoaji wa elimu bora ili kupata wahitimu mahiri wa kuja kulitumikia taifa katika nyanja mbalimbali za kijamii, kisiasa na kiuchumi.

Wanapotoa mihadhara wazingatie mahitaji ya wanafunzi kwani wapo wengine wanaoelewa kwa kasi lakini pia kuna kundi la wanaoelewa taratibu lakini wote wanahitaji kusoma na kuelewa.

Hivyo basi, kiu ya kufidia muda uliopotea isihatarishe uelewa wa wanafunzi kwa kufundisha kwa kasi kubwa kupewa kazi nyingi za kufanya kwa wakati mmoja kwani itawafanya wanafunzi wengine kushindwa kuelewa na hivyo kufeli mitihani yao na hata kukwama kimaisha chanzo kikiwa ni tatizo la corona.

Katika kuhakikisha kuwa wanafunzi wanapata maarifa bora baada ya kufunguliwa kwa vyuo, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia iliwakutanisha wakuu wa vyuo vikuu vyote nchini ili kuweka mkakati wa pamoja wa namna ya kufikia malengo ya ufundishaji na ukamilishaji wa mitaala baada ya kufungua vyuo Juni 1, 2020.

Katika mkutano huu, vyuo viliweka mikakati ya pamoja ili kwenda pamoja kwenye kufidia muda uliopotea na kukamilisha mihula bila kuathiri maendeleo ya taaluma na mustakabali mwema wa elimu kwa wanafunzi na taifa.

Mwenyekiti wa Kamati ya Wakuu wa Vyuo (CVCPT) ambaye ni Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Profesa Raphael Chibunda, aliihakikishia Wizara ya Elimu kuwa watakwenda kutekeleza mikakati iliyofikiwa ili kuwasaidia wanafunzi katika vyuo mbalimbali kufidia muda uliopotea na kupata elimu bora ili kuyafikia malengo yao.

Sambamba na hilo, mkutano huo unaazimia vyuo kuendelea kuchukua tahadhari ya ugonjwa wa corona kwa kuhakikisha wanafunzi wanavaa barakoa na kila chuo kuweka mazingira mazuri kwa wanafunzi kunawa mikono kwa sabuni na maji tiririka kila wanapoingia na wawapo darasani na kutoka masomoni na katika mazingira yote ya chuo na mabweni ili wanafunzi wawe salama kiafya.

Wanafunzi waendelee kusoma kwa bidii na kwa juhudi kubwa kwani wana malengo wanayotaka kuyafikia kupitia elimu.

Pamoja na changamoto ya corona, maisha mengine lazima yaendelee tena kwa mafanikio makubwa. Viongozi na wadau wa elimu waendelee kuweka mikakati kwa upande wa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne namna bora ya kuwasaidia watakaporejea shuleni.

Lengo ni kuhakikisha muda uliopotea unafidiwa kwa kutumia mbinu mbalimbali ili wanafunzi wapate maarifa, ujuzi na stadi bora za kuwasaidia katika masomo yao.

Msisitizo pia uwekwe katika kuandaa vifaa vya kutosha vya kujikinga na corona kama vile sabuni na maeneo ya kutosha ya kunawa mikono ili afya za wanafunzi na walimu ziendelee kuwa salama.

**Reubeni Lumbagala ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko Dodoma.**
**Maoni: 0765-409249.**

SAYANSI

NA MOHAMMED SHARKSY, ZANZIBAR



Kunyonyesha ni tija kwa watoto, wazazi na nchi ndiyo maana kinamama mwezi huu wanakumbushwa tena kuwanyonyesha watoto kwa upendo. **PICHA: MTANDAO.**

## KUNYONYESHA

# Ni mlolongo wa faida mtoto, wazazi, taifa

KILA mwaka ifikapo Juni mosi, ni siku ya kimataifa ya unyonyeshaji maziwa ya mama ambayo ni msingi na muhimu kwa afya ya mtoto kutokana na faida nyingi yaliyo nayo.

Ni mwezi wa kunyonyesha hivyo ndivyo ulivyo umuhimu wa kuhimiza unyonyeshaji wa maziwa ya mama na faida zake kwa mama, mtoto, baba na jamii.

Kutokana na utandawazi kuna madai kuwa wapo baadhi ya kina mama wazazi ambao hawanyonyeshi watoto ipasavyo, wanaelezwa kuwa ni miongoni mwa wale wenye umri wa miaka 20 mpaka 35. Wanadaiwa kuwa wana hofu kwamba maziwa yao yatalala au kuanguka na kupoteza haiba katika jamii au labda watakataliwa na wenza wao.

Jambo hili linasikitisha kwani kunyonyesha ni njia mojawapo muhimu inayomuunganisha mama na mtoto, na iwapo mtoto hatanyonya, ni wazi hata ule ukaribu na mama pia hautakuwapo.

Kunyonyesha ni pale mama mzazi anapompa mtoto maziwa kutoka katika matiti yake moja kwa moja au kumnywesha mtoto maziwa yake yaliyokamuliwa kwa kutumia kikombe au chupa zilizoandaliwa kwa ajili ya kuwanyonyesha watoto wachanga na wadogo.

Ni vyema kukumbuka na kuzingatia kuwa maziwa ya mama ni chakula na kinywaji cha kwanza na cha pekee kwa mtoto mara tu anapozaliwa mpaka kufikia umri wa miezi sita bila kumpa hata maji.

> “Unyonyeshaji bora wa maziwa ya mama hujenga uhusiano wa karibu kati ya mama na mtoto na humpatia kinga dhidi ya maradhi mbalimbali kama kuharisha, magonjwa ya njia ya hewa na masikio.

Shirika la Afya Duniani (WHO) na Shirika la Kuhudumia Watoto la Umoja wa Mataifa (Unicef), yanapendekeza mtoto aanze kunyonya maziwa ya mama saa moja baada ya kuzaliwa.

Ndicho chakula bora kwa mtoto mchanga kuliko maziwa mengine yoyote yale au chakula chochote.

Maziwa ya mama ni chakula halisi cha kwanza kwa watoto, na yanawapatia virutubisho vyote vinavyohitajika katika miezi ya mwanzo ya maisha yao.

Mtoto afikishapo umri wa miezi sita apewe vyakula vingine laini vya nyongeza huku akiendelea kunyonyeshwa maziwa ya mama hadi atimize miaka miwili au zaidi na hayo yako kwenye baadhi ya vitabu vitakatifu.

Vinavyoelekeza kuwa mtoto anyonyeshwe maziwa ya mama kwa kipindi cha miaka miwili mfululizo.

Kunyonyesha ni njia moja sahihi ya kuhakikisha mtoto anakuwa mwenye afya nzuri na kuendelea kuishi katika hali bora.

Kwa maana hiyo ziko faida lukuki anazopata mtoto, mama na baba na jamii pia.

**MANUFAA KWA MTOTO**

Kumnyonyesha mtoto mara anapozaliwa kwa kipindi cha saa moja, humkinga na maambukizo yanayowapata watoto wakiwa wachanga hivyo kupunguza vifo vya watoto hawa.

Virutubisho vinavyopatikana kwenye maziwa ya mama, mchanganyiko wake ni wa kimaumbile zaidi. Kwa vile yanatolewa kiasili, hayana gharama yoyote, na ni salama zaidi.

Yanaleta manufaa ya kisaikolojia vilevile, yanasaidia kujenga uhusiano mzuri kati ya mama na mtoto wake mchanga.

Humpatia vyakula vyote sita vinavyojenga mwili na virutubisho vyote na vitamini anavyohitaji kwa uwiano ulio sahihi kwa ukuaji na maendeleo yake kama vile protini, vitamin, wanga, sukari, maji na madini.

Unyonyeshaji bora wa maziwa ya mama hujenga uhusiano wa karibu kati ya mama na mtoto na humpatia kinga dhidi ya maradhi mbalimbali kama kuharisha, magonjwa ya njia ya hewa na masikio.

Maziwa ya mama humwezesha mtoto kukua kimwili na kiakili kwa ukamilifu.

Maziwa ya mama huleta uhusiano mzuri na wa karibu kati ya mama na mtoto.

Mtoto aliyenyonya maziwa ya mama huwa na mwenendo mzuri pamoja na akili ukilinganisha na yule asiyenyonya maziwa ya mama.

Maziwa ya mama humweka mtoto salama na mwenye joto la kutosha akiwa pembeni mwa mama yake.

Aidha, unyonyeshaji wa mtoto humsaidia kuboresha uwezo wa utambuzi wa akili (IQ), mahudhurio ya shule na pia huhusishwa na mapato ya juu katika maisha yake ya utu uzima.

Maziwa ya mama ni kinga inayodumu muda mrefu dhidi ya ugonjwa wa kisukari, mzio na saratani mbalimbali katika maisha ya mtoto ya baadaye.

**MAMA NAYE**

Maziwa ya mama huchangia katika kulinda afya yake kwa njia mbalimbali mathalani, kurudisha tumbo la uzazi.

Mama anaponyonyesha mara baada ya kujifungua husaidia tumbo la uzazi kurudi katika hali ya kawaida mapema.

Aidha, husaidia kudhibiti na kupunguza utokaji wa damu hivyo kuzuia upungufu wa damu.

Maziwa ya mama hupunguza uwezekano wa kupata ujauzito katika miezi sita ya mwanzo kama mama atamnyonyesha mtoto maziwa yake tu mara nyingi kwa siku na pia kama hajapata hedhi.

Hupunguza uwezekano wa kupata saratani ya mfuko wa uzazi na matiti lakini pia hujenga uhusiano wa karibu kati ya mama na mtoto.

Iwapo mama aliongezeka uzito mwingi wakati wa mimba, kunyonyesha husaidia kumrudishia umbile lake la kawaida.

Mama anapomnyonyesha mtoto hujengeka kiafya na kisaikolojia na mapenzi ya hali ya juu.

**NAFASI YA BABA**

Maziwa ya mama gharama yake ni nafuu. Hakuna haja ya kununua vyakula mbadala, chupa, au chochote kingine kwa hiyo baba hatatumia rasilimali za ziada kumlisha mtoto vyakula vya viwandani.

Kwa vile maziwa ya mama ni kinga ya kutosha kwa mtoto itampunguzia baba kutumia fedha kwa ajili ya matibabu ya mtoto.

Baba atapata muda wa kutosha wa kuhudumia watoto wengine katika huduma muhimu kna chakula, matumizi ya shule na mavazi kwa jumla.

**FAIDA KITAIFA**

Ikiwa watoto watanyonyeshwa kikamilifu kutakuwa na punguzo kubwa la gharama ya matibabu hasa kwa wale wenye chini ya miaka mitano kwani watakuwa wamejengeka vyema afya zao dhidi ya maradhi ambukizo na yasio ambukiza.

Ni uhakika wa nguvu kazi yenye uwezo wa kutumikia taifa kutokana na kuwa na afya zilizoimarika.

**MANUFAA YALIKO**

Mtoto afikishapo umri wa miezi sita aanzishwe chakula cha nyongeza huku akiendelea kunyonya maziwa ya mama yake kwa mpangilio mzuri.

Baada ya miezi sita apewe chakula cha nyongeza kwa kupima kwa kutumia kikombe, au kipimo kingine, kijiko na ni vizuri kuepuka matumizi ya chupa.

Vyakula vya nyongeza viwe ni vya mchanganyiko wa makundi yafuatayo ya vyakula vya nafaka, mizizi na aina za viazi nyama, mboga na matunda, mafuta na sukari kwa kiasi kidogo.

Mtoto aendelee kunyonya mpaka afikie umri wa miaka miwili au zaidi na unyonyeshaji bora wa maziwa ya mama ndiyo njia pekee ya kumpa chakula na kinywaji mtoto wako. Inawezekana timiza wajibu.

**Mwandishi ni Mkufunzi Msaidizi,**
**Shule ya Afya Sayansi za Tiba, Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar- SUZA**
**0777432493, mohammed.rashid96@yahoo.com, rurumа96**

ELIMU

## NA SABATO KASIKA

# Motisha yaichomoa shule toka mkiani hadi 10 bora

BAADHI ya shule nchini zinakabiliwa na changamoto ambazo wakati mwingine husababisha ziwe na matokeo mabaya katika mitihani na maendeleo ya taaluma, lakini si kwamba matatizo hayo hayatatuliki yako ndani ya uwezo wa jamii.

Motisha kwa walimu na wanafunzi ni moja ya njia zinazoweza kutumia na jamii kumaliza baadhi ya changamoto katika shule na kupandisha ufaulu, kwa vile huwafanya walimu wafundishe kwa moyo.

Halmashauri ya Madaba mkoani Ruvuma, imeligundua hilo na kulifanyia kazi na sasa ufaulu wa shule za sekondari katika halmashauri uko juu.

Hivyo ndivyo, Ofisa Elimu -Sekondari Halmashauri ya Madaba, Michael Hadu, anavyosema katika mazungumzo na Nipashe kuhusu maendeleo ya elimu.

"Motisha kwa walimu na wanafunzi imekuwa chachu ya maendeleo ya elimu katika wilaya ya Madaba na halmashauri kwa ujumla na hii imeongeza ufaulu na kutuinua kimkoa na kitaifa," anasema Hadu.

Kwa mujibu wa Hadu, Madaba ina shule nane za sekondari zikiwamo tatu za binafsi huku za msingi zikiwa 28 na moja ni ya binafsi.

Ofisa elimu huyo anasema, utaratibu wa motisha kwa walimu na wanafunzi ulianza mwaka 2017 ambapo wote wamekuwa wakipata chai shuleni na vitu vingine vya muhimu na hivyo kila upande kufanya kazi kwa umakini.



Mdau wa elimu, Joseph Mhagama (kushoto), akikaribishwa katika moja ya shughuli za kuhamasisha maendeleo ya elimu katika shule za msingi na sekondari wilayani Madaba. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

**KUPANDISHA UFAULU**

Kutokana na motisha hiyo, anasema ufaulu wa wanafunzi katika Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Pili umepanda kutoka nafasi ya 104 mwaka 2018 hadi nafasi ya 24 mwaka 2019 na kushika nafasi ya kwanza kimkoa.

"Si hao tu bali hata kidato cha sita mwaka 2019 katika Shule ya Sekondari ya Madaba, wanafunzi 23 wamepata daraja la kwanza, hivyo tumeshika nafasi ya saba kati ya shule 26 za mkoa wa Ruvuma," anasema.

Ofisa Elimu huyo anaeleza kuwa hata katika mtihani wa taifa wa kidato cha nne, Halmashauri ya Madaba imefanya vizuri na kushika nafasi ya 23 kitaifa mwaka 2019 huku ikiwa ya kwanza kimkoa.

"Haya ni mafanikio ya kutoka nafasi ya 121 kitaifa mwaka 2018 na hii yote imechangiwa na juhudi za wadau wa elimu akiwamo mbunge wa jimbo la Madaba, Joseph Mhagama," anasema.

**KERO ZA MWALIMU**

Ofisa Elimu Hadu anasema Mbunge wa Jimbo la Madaba, Mhagama, ni mdau wa elimu ambaye amekuwa akipita katika shule na kusikiliza kero za walimu na kuwatia moyo huku akiwasisitiza kuwafundisha kwa upendo na kufanya kazi kwa bidii.

"Wadau wa aina hii ni muhimu katika elimu kwa ajili kuhamasisha na kuchochea ari ya walimu kufundisha na wanafunzi kujifunza na pia kushirikiana na wananchi kujenga mabweni na madarasa.

Anasema, Wilma Sekondari imeshika nafasi ya nane na kuingiza shule zao mbili za kidato cha sita katika 10 bora ikiwamo Madaba Sekondari kwa mara ya kwanza ikiwa ni ufuatiliaji wa wataalamu kwa kushirikiana na mbunge.

Hadu anasema, anaamini kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi wa shule za sekondari na msingi katika jimbo la Madaba kitazidi kupaa iwapo wadau zaidi wa elimu wataendelea kujitokeza.

"Mbali na hayo, serikali imetuletea madawati 251 yaliyosambazwa katika shule za msingi na chache za sekondari, lakini gharama za kuyasafirisha Sh. 534,000 zilitolewa na mbunge," anasema.

**MOTISHA**

Ofisa elimu huyo anasema, motisha ilianzishwa na mbunge Mhagama mwaka 2017 kwa kutoa Sh. 500,000 kwa kila shule ya sekondari ili kusaidia walimu na wanafunzi kupata kifungua kinywa shuleni.

Mbali na kiasi hicho cha fedha, anasema mbunge huyo pia amekuwa akiwapa walimu sukari ya mwaka mzima kwa matumizi yao nyumbani ikiwa ni motisha ili wafanye kazi kwa bidii.

"Motisha hiyo imekuwa chachu ya maendeleo ya elimu katika jimbo la Madaba, na hali hii imeongeza ufaulu na kutuinua kimkoa na kitaifa, na pia ni wito wangu kwa wadau wengine kuunga mkono juhudi hizi," anasema.

Anasema, tangu mbunge huyo alipoanza kuweka msukumo huo kwa ajili ya halmashauri na jimbo hilo sambamba na kuhakikisha kunakuwapo ongezeko la viti, meza, vitabu na vifaa vingine vya kufundishia na kujifunzia, maendeleo ya kielimu yamebadilika.

"Niseme kwamba amekuwa na mchango mkubwa kwa Idara ya Elimu katika jimbo na halmashauri ya Madaba kwani pia amesaidia kufuatilia na kutuletea Sh. milioni 240 kwa ajili ya ujenzi wa maabara," anasema.

**ZAWADI KWA WALIMU**

Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Mahanje, Makoye Richard, anasema motisha kwa walimu imeongeza ari ya ufundishaji kwa walimu na kuongeza ufaulu shuleni kwake.

> "Motisha hiyo imekuwa chachu ya maendeleo ya elimu katika jimbo la Madaba, na hali hii imeongeza ufaulu na kutuinua kimkoa na kitaifa, na pia ni wito wangu kwa wadau wengine kuunga mkono juhudi hizi," anasema.

"Ufaulu wa daraja la kwanza na la pili ulikuwa ndoto kwa shule yetu, lakini kwa mara ya kwanza, wanafunzi 48 waliofanya mtihani wa taifa wa kidato cha nne, mmoja alipata daraja la kwanza, sita wakapata daraja la pili, wengine 14 daraja la tatu na 26 wakapata daraja la nne," anasema Richard.

Anasema, walimu wa shule ambazo hufanya vizuri pamoja na wanafunzi wao, huwa wanapata zawadi ya Sh. Sh 300,000 kila mmoja na vifaa vya kujifunzia na kufundishia kutoka kwa mbunge.

"Hatua hiyo na ushirikiano mzuri kati ya wazazi, walimu na mbunge wao umewafanya wanafunzi kuongeza bidii na umakini, na sasa karibu nusu ya darasa wanafaulu na kujiunga na kidato cha tano," anasema.

Mwalimu huyo anasema, hata wanafunzi wengine wanaobaki, nao wanaenda katika vyuo mbalimbali, na kwamba shuleni kwake mbunge anahakikisha wanafunzi wa kike wanapata taulo za kike.

"Kuwapo kwa taulo hizo kumeongeza mahudhurio katika vipindi vyote vya masomo hata wakati wakiwa kwenye hedhi na kuwafanya waongeze umakini katika masomo," anasema.

TEKNOLOJI

NA GAUDENSIA MNGUMI

# Simujanja ilivyommaliza ofisa wa polisi Marekani

BINTI wa miaka 17, Darnella Frazier, ndiye aliyepiga picha kwa simu janja na kurekodi ukatili wa ofisa wa polisi katika jiji la Minneapolis, David Chauvin, akimkandamiza kwa goti kwenye mshipa mkuu hadi kumwua George Floyd, Mwamerika mweusi hivi karibuni.

Darnella anauambia mtandao wa TMZ kuwa anajuta kutokana na kusambaza ujumbe huo wa mauaji kwa baadhi ya marafiki zake kutokana na vituko na vitisho anavyopokea sasa.

Anaeleza kuwa analaumiwa zaidi kuwa alishindwajea kutetea maisha badala yake alikuwa akipiga picha na kurekodi tukio.

Alirekodi mkanda huo ambao unaonyesha Chauvin akimkandamiza kwa goti kwa dakika nane Floyd hadi alipofariki dunia huku maofisa wengine wakiangalia bila kujali kuwa kilikuwa kitendo cha mauaji.

"Kama siyo mimi polisi walikuwa wanaendelea na kazi zao na kusababisha matatizo mengine.

Video yangu imesambaa dunia nzima kwa kila mmoja kuona na kuujua ukweli .Hata familia yake ilifikiwa na taarifa hizo. Badala ya kuniponda nishukuruni mimi THANK ME."


Teknolojia ya simujanja ndiyo iliyofanikisha polisi kushitakiwa kwa mauaji, kwani Jumatatu iliyopita polisi Mzungu nchini Marekani aliumua kikatili Mmarekani mwenye asili ya Afrika katika mji wa Minneapolis, jimbo la Minnesota na kilichomuibua ni video iliyosambaa kwenye mitandao ya kijamii nchini humo na duniani kote na kudhihirisha tena umuhimu wa simu janja.

Simu ya binti huo ilipiga picha iliyomuonyesha polisi mzungu akiwa amemlaza na kuficha chini ya gari Floyd akiwa kifudifudi huku akiwa amemkandamiza vibaya shingo yake kwa goti la mguu wa kushoto.

George Floyd alikuwa akipiga kelele kwa kusema:"Umenibana shingo siwezi kupumua" "naomba maji" "usiniue" Polisi huyo hakujali hadi alipofariki dunia.

Kufuatia ukatili huo wa kutisha, Meya wa mji wa Minneapolis, Jacob Frey, aliwafukuza kazi maofisa wanne wa polisi kwa kusababisha kifo cha Floyd.

Vitendo vya ukatili wa polisi wa Marekani dhidi ya Wamarekani Weusi, vimekuwa vikiibua maandamano na malalamiko ya raia wa nchi hiyo. Mauaji dhidi ya Wamarekani weusi nchini humo yanayofanywa na polisi yalishika kasi kuanzia mwaka 2014 suala ambalo limeibua harakati za kiraia pamoja na vitendo vya utumiaji mabavu na hata machafuko ya siku kadhaa katika majimbo kadhaa ya nchi hiyo kutokana na kusambaa nchi nzima.



Darnella Frazier, aliyepiga picha kwa simu janja na kurekodi ukatili wa ofisa wa polisi katika jiji la Minneapolis, David Chauvin, akimuua Floyd. Binti huyo anadai kufedheheka kutokana na wengi kumlaumu. **PICHA: MTANDAO**

> "Video yangu imesambaa dunia nzima kwa kila mmoja kuona na kuujua ukweli .Hata familia yake ilifikiwa na taarifa hizo. Badala ya kuniponda nishukuruni mimi THANK ME."

Licha ya teknolojia kufanyakazi yake, ya kutoa ushahidi usio na shaka lakini imekuwa ni jambo la kawaida mahakama za Marekani huwa zinawaachilia huru polisi wanaotenda jinai dhidi ya Wamarekani weusi au kuwapa adhabu hafifu ikilinganishwa na makosa waliyofanya.

Lakini yote hayo huenda sasa yakapungua kutokana na teknolojia ya simu janja ambayo imefanikisha muaji ya Floyd kutiwa mbaroni na kushtakiwa kwa kosa la mauaji ya kukusudia na kuua kwa uzembe raia ambaye hakuwa na silaha.

Ndugu wa marehemu Floy aliyekuwa na umri wa miaka 46, ambao walizungumza na Rais Donald Trump, wameonyesha kuridhishwa na hatua ya kukamatwa kwa ofisa huyo kama uelekeo wa upatikanaji wa haki, lakini pia wanasema wana matumaini ya kufunguliwa zaidi kwa mashitaka makali na hatua dhidi ya maofisa wengine ambao wamehusika na kumweka kizuizini Floyd na hatimae kifo chake.

Teknolojia ya simu janja imewezesha dunia kuwa na ugunduzi zaidi mapinduzi yanayokuza na kuimarisha njia za mawasiliano yanayounganisha mamilioni ya watu kwa sekunde chache kote duniani.

Simu janja zina huduma ya facebook, twitter, intagram na viber ambayo ni njia ya kupiga simu kwa mtandao au skype.

Yote haya yanafanikisha usambazaji wa taarifa kwa kasi dunia nzima na pia kuibua mambo ambayo bila kuwapo kwa simu hizo au pengine kutumia kamera za video za kawaida yasingeweza kuripotiwa.

Kwa Tanzania simu hizo zimetumika kuwajibisha askari wanaoomba na kupokea mlungula hasa barabarani.

Aidha, zimedhibiti uhalifu shuleni walimu wanaotandika wanafunzi na kuwaadhibu kupindukia na hata kuwaumiza nao wameibuliwa.

Simu hizo zimetumika kuwatia hatiani wahalifu wakiwamo wanaopanga na kufanikisha mauaji.


Hata hivyo, kuna wengi wanaodhani kuwa simu hizo si 'janja' kwa vile zinatumiwa kusambaza habari za uongo na uzushi.

Hilo linatokea na kuna kipindi unyanyasaji wa wanawake kimtandao ulizidi na kusababisha wengi kujiua kwa kuogopa aibu na kashfa za maisha yao zilizojaa mitandaoni.

Hata hivyo, kuna sheria za kufuatilia na kudhibiti unyanyasaji huo. Na ni kwa nadra wahusika wanaendeleza mambo hayo.

Na kwa ujumla licha ya umuhimu wa simu hizo kumeibuka uteja. Watu wengi wanapenda simu kuliko familia zao, watoto, wapenzi na hata kazi zao.

Simu za mikononi zinawafanya wengi kuwa tegemezi wa whassao, tweeter, facebook na pengine miaka inavyokwenda usomaji vitabu utatoweka badala yake simu za mikononi zitakuwa rafiki na kipenzi namba moja wa mwanadamu.




Chauvin akimkandamiza kwa goti kwenye mshipa mkuu hadi kumwua George Floyd, Mamerekani mweusi hivi karibuni. **PICHA: MTANDAO.**





# Wenye ulemavu ngozi wataka ulinzi kuelekea uchaguzi mkuu

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WATU wenye ulemavu wa ngozi mkoani Dodoma, wameiomba serikali kuimarisha ulinzi kwao kuelekea uchaguzi mkuu wa mwaka huu, kutokana na ukatili ambao umekuwa unafanywa dhidi yao wakati wa uchaguzi.

Wamesema kuwa wakati wa mchakato wa uchaguzi, wamekuwa wakiuawa, kukatwa viungo na kufukuliwa makaburi wanayozikwa kwa imani ya ushirikina.

Mwasisi wa taasisi isiyo ya kiserikali inayojihusisha na masuala ya utetezi wa haki na usawa kwa watoto (FDH), Maiko Hosea, alitoa rai hiyo mwishoni mwa wiki wakati akitoa taarifa kwa vyombo vya habari juu ya maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Kuongeza Uelewa kuhusu Ualbino yatakayofanyika kitaifa Juni 13, mwaka huu, mkoani hapa.

Hosea alisema kuwa katika kipindi cha uchaguzi, vitendo vya ukatili vimekuwa vikijitokeza dhidi yao na kuwasababishia kuishi kwa wasiwasi mkubwa kutokana na unyama huo wa kuuawa, kukatwa viungo na hata kufukuliwa makaburi yao.

Alisema kuwa wakati wa uchaguzi nchini unapowadia, unakuwa mgumu kwao kutokana na ukatili wanaofanyiwa wa kuwindwa kama digidigi kutokana na imani za ushirikina, hivyo akaiomba serikali na wananchi kuhakikisha wanawalinda watu wenye ualbino.

"Ukatili dhidi ya watu wenye ualbino tumeona ukiendelea, ukifanyika wakati wa uchaguzi mkuu wa viongozi. Kwa mfano, tumeona kule mkoani Mbeya ambako watu wamefukua makaburi, tumeona ukatili ukiendelea kufanyika na tumeona unyanyasaji ukifanyika wa kutegwa na jamii pia, hivyo tunaomba serikali na wazazi kuweka ulinzi wa kutosha," alisema.

Mwasisi huyo pia alisema kuwa pamoja na jitihada za serikali kutatua tatizo la upatikanaji wa mafuta ya kujikinga na saratani ya ngozi, bado ni kikwazo kwao katika kuwafikia walengwa kutokana na hali halisi ya umaskini na ukosefu wa ajira kwa watu wenye ualbino.

Mkurugenzi wa taasisi hiyo, Epiphania Kabunduguru, alisema maadhimisho hayo ya tano ya kimataifa na ya 16 kitaifa, mwaka huu yataongozwa na kauli mbiu ya 'Utu Wako, Maisha Yangu'. Alisema bado kuna tatizo kwa baadhi ya wazazi na walezi kutowalinda watoto wenye ualbino kwa kuwapatia mavazi stahili na mafuta.

Ofisa Idara ya Utawala wa Taasisi hiyo, Elizabeth Msuya, alisema kuwa wamejipanga kutoa elimu kwa wazazi na walezi juu ya kuwalinda kiafya watoto, ikiwa na pamoja kuwasisitizia vijana kujihusisha na ujasiriamali na utetezi kwa watu wenye ualbino.



Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Mwingulu Nchemba (kulia), akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake, eneo la Mtumba, jijini Dodoma juzi, kuhusu upotoshwaji wa ukweli wa haki za binadamu nchini, unaofanywa na baadhi ya watu. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## 'Machinga watumie fursa vitambulisho ujasiriamali'

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

OFISA Masoko wa Jiji la Dodoma, James Yuna, amewataka viongozi wa wafanyabiashara wadogo (machinga), kuwahamasisha wenzao kuchangamkia vitambulisho vinavyotolewa na serikali kwa ajili ya ujasiriamali.

Alitoa rai hiyo jana alipozungumza na uongozi wa wafanyabiashara ndogo kwenye kikao cha pamoja kilichofanyika Soko Kuu la Majengo jijini, akisema viongozi hao wana nafasi kubwa ya kuwaelimisha na vitambulisho hivyo wakavipata kwa wakati.

Alisema vitambulisho hivyo vimeanza kutolewa kwa lengo la kuwasaidia vijana ambao wanajishughulisha na ujasiriamali, kufanya shughuli zao bila kubugudhiwa na kupoteza mali.

Alisema kuwa kwa mantiki hiyo, viongozi wana wajibu mkubwa wa kutoe elimu ambayo itahamasisha uchukuaji wa vitambulisho hivyo kwa lengo la kuiunga mkono serikali ambayo imewataka kuwa navyo.

"Ni imani yangu kuwa ninyi kama viongozi wa machinga wa Jiji la Dodoma, mtahakikisha mnahamasisha wafanyabiashara ndogo, kila mmoja wapo anakuwa na kitambulisho cha ujasiriamali vilivyotolewa na serikali kwa ajili yenu," alisema.

Katibu wa Machinga Wilaya ya Dodoma, Anna Ndaga, alisema vitambulisho hivyo vilivyotolewa na serikali kwao ni muhimu na wana kila sababu ya kuishukuru serikali kwa kuwa vitawawezesha kufanya shughuli zao za kibiashara kwa uhuru bila kubugudhiwa.

Aliwataka wafanyabiashara wadogo kuheshimu maeneo yasiyoruhusiwa na jiji kufanya biashara zao kwa kuwa kutoyatii, kutasababisha migogoro isiyo ya lazima kati yao na Halmashauri ya Jiji.

Alisema baadhi yao wamekuwa wakifanya biashara maeneo hatarishi ambayo siyo rafiki kwao, wateja wao na hata bidhaa zao, hali ambayo imekuwa ikisababishia kupata hasara pindi wanapotakiwa kuondoka kwa kushurutishwa.

# Waziri ataka vituo uuzaji ufuta

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Kilimo, Japhet Hasunga, ameuagiza uongozi wa Mkoa wa Dodoma kuanzisha vituo vya kununua zao la ufuta kwa utaratibu wa stakabadhi ghalani katika vijiji vyote vinavyozalisha.

Vilevile, ameagiza kutafuta wanunuzi wa uhakika waliosajiliwa na serikali na kuhakikisha malipo yote ya fedha za wakulima yasizidi siku tatu baada ya mauzo.

Waziri Hasunga alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki kufuatia malalamiko ya wakulima kuhusu utaratibu huo mpya wa ununuzi wa zao hilo, wakidai serikali bado haijajipanga kwa kuwa hakuna vyama vya ushirika ambavyo ndiyo wasimamizi wakuu wa mfumo wa stakabadhi ghalani.

Akizungumza na wakulima kwenye Kijiji cha Pahi wilayani Kondoa, Waziri Hasunga alisema nia ya serikali ni kuona wananchi wake wananufaika na jasho lao kwa kuwatafutia masoko ya uhakika.

Alisema kuwa lengo lao ni kuona wakulima wote wananufaika na kile walicholima na siyo kulalamika kutokana na kukosa masoko na fedha zao kucheleweshwa.

Alisema mkoa unaweka utaratibu wa kununua ufuta ili wakulima nao wafaidike na zao ambalo wamelima kama zao la biashara.

"Ninaomba agizo hilo litekelezwe, sihitaji kuona au kusikia wakulima wa ufuta wanalalamika," Hasunga aliagiza.

Kabla ya kutoa tamko hilo, baadhi ya wakulima, akiwamo Maulid Dunga na Haruna Mwinjuma, walilalamika kuwa mfumo huo umekuja ghafla bila kushirikishwa na kuzua hofu ya baadhi ya watu wenye nia mbaya kuhujumu mazao yao.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, aliahidi kukutana na halmashauri zote zinazolima zao hilo, pamoja na wawakilishi wa wakulima, ili kuwa na mipango ya pamoja ya ununuzi ambayo haitaathiri upande wowote.

Alisema wakulima wanapaswa kuondoa wasiwasi kwa kuwa mkoa utatekeleza kile alichoagiza waziri mwenye dhamana ya kilimo.

Alisema Mkoa wa Dodoma kupitia Wilaya za Bahi, Chamwino na Kondoa unazalisha zao la ufuta kwa kiasi kikubwa ambapo katika msimu huu wa kilimo, bei ya soko kupitia mfumo wa stakabadhi ghalani imefika Sh. 2,250 kwa kilo.

# Upatikanaji majisafi wakwamisha unawaji mikono

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

WAKAZI wa Vijiji vya Madundasi na Iyala, Kata ya Luhanga, Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, mkoani Mbeya, wanakabiliwa na tatizo la upatikanaji wa majisafi na salama kwa kipindi kirefu hali inayosababisha unawaji mikono kwa maji na sabuni kuwa gumu katika kipindi hiki cha ugonjwa wa Covid-19.

Wakizungumza na Nipashe juzi, wakazi hao walisema hawana chanzo cha uhakika cha maji na badala yake hutembea umbali mrefu kufuata maji ya mito na visima ambavyo vilijichimba kipindi cha mvua za masika.

Mmoja wa wakazi hao anayetoka Kijiji cha Madundasi, Tatu Shinamwalenga, alisema maji yanayopatikana yanatosha kwa kupikia, kunywa na kuosha vyombo.

"Tunashindwa kufuata maelezo ya wataalamu wa afya yanayotaka tuwe na utamaduni wa kunawa mikono kwa maji tiririka na sabuni mara kwa mara ili kujikinga na ugonjwa wa Covid-19," alisema Shinamwalenga.

Alisema maji wanayopata kwenye mito na visima hivyo ni ya foleni na wanalazimika kuamka saa tisa ya usiku kuyafuata, wakati mwingine hulazimika kununua ndoo moja kwa Sh. 500 ambayo ni maalum kwa ajili ya kunawa hasa maeneo ya biashara kama vile migahawa.

Theresia Joseph, mkazi wa Kijiji cha Iyala, alisema kuna uhaba mkubwa wa maji mvua za masika zinapokata na visima wanavyovitegemea vimeanza kukauka na kuhatarisha kukosekana huduma hiyo.

Alisema unawaji mikono ili kujikinga na maambukizo ya ugonjwa wa Covid-19 ni mgumu licha ya kuwa wanalazimika kuingia gharama ya kununua maji ili kutekeleza agizo hilo.

"Kama tulivyoelekezwa na wataalamu wa afya katika vita dhidi ya corona, inatubidi tunawe mikono kwa maji na sabuni mara kwa mara, sasa kwa tatizo la maji hapa kwetu ni vigumu kulitekeleza suala hili kama inavyotakiwa na mbaya zaidi tunaelekea msimu wa kiangazi kufika Septemba, maji yote ya mito na visima yatakauka, sijui endapo ugonjwa wa corona ukiendelea hali zetu zitakuaje," alisema Joseph.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Madundasi, Ismail Chungu, alisema maji wanayotumia wananchi wake sio safi na salama kwa sababu huchangia na mifugo.

Alisema maji yanayotumiwa yanatoka kwenye mifereji iliyojengwa wa ajili ya kumwagilia mpunga mashambani na kero hiyo ilifikishwa kwenye uongozi wa wilaya wanachosubiri ni utekelezaji.

Katika kukabiliana na tatizo la maji vijijini, serikali ilianzisha Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (Ruwasa), ambao ulipewa kazi ya kujenga, kukarabati na kupanua miundombinu ya maji, kujenga visima pamoja na mabwawa.

Meneja wa Ruwasa, wilayani Mbarali, Mhandisi Jobu Mwakasala, alisema wanafahamu adha wanazozipata wananchi wa vijiji hivyo na hatua zilizochukuliwa tangu mwaka 2010 ni kusanifu mradi wa Luhanga, ambao kutokana na ukata wa fedha haukukamilika kwa wakati.

Alisema Ruwasa kwa sasa wamejipanga kuupitia upya na kuukamilisha mradi huo ambao utahudumia vijiji vyote vya kata hiyo na kuwakumbusha wananchi kuuchukulia ugonjwa huo kama dharura ambayo ni vita, hivyo kila mmoja atumie maji yaliyopo kunawa mikono ili kujikinga.

Mganga Mkuu wa Wilaya hiyo, Dk. Godfrey Mwakalila, aliwashauri wakazi hao kuendelea kuvitumia vyanzo vya maji vilivyopo kunawa mikono kwa kuwa kinachohitajika ni kupata povu la sabuni ambalo linahitajika kusafisha mikono bila kujali ni maji ya namna gani.



Mwenyekiti wa Chama cha Waandishi wa Habari Mkoa wa Mbeya (MBPC), Festo Sikagonamo (kushoto), akikabidhi vifaa vya kujikinga na maambukizo ya ugonjwa wa corona, ambavyo ni vitakasa mikono, glovu, sabuni na barakoa, kwa mwanachama Kakuru Msimu, ambavyo vilitolewa na Umoja wa Vilabu vya Waandishi wa Habari nchini UTPC, jijini Mbeya juzi. **PICHA: GRACE MWAKALINGA.**

# Bil. 4/- zatumika kuboresha miundombinu umwagiliaji

**Na Grace Mwakalinga,** MOMBA

JUMLA ya shilingi bilioni nne zimetumika kuboresha miundombinu ya sekta ya kilimo cha umwagiliaji wa zao la mpunga katika Skimu ya Naming'ong'o, Kata ya Chitete, Halmashauri ya Momba, mkoani Songwe ili kuongeza tija katika uzalishaji.

Fedha zilizotolewa na serikali zililenga kujenga na kuboresha miundombinu ya umwagiliaji kwenye zao la mpunga ambalo kwa sasa ni tegemeo kwenye halmashauri hiyo kutokana na wakulima wengi kujikita kwenye zao hilo.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi, Ofisa Mipango wa wilaya hiyo, Geofrey Mwambasa, alisema kwa kutambua umuhimu wa zao hilo ambalo kwa sasa ndio tegemeo, serikali ilitoa kiasi hicho cha fedha ili kuboresha miundombinu ikiwamo ujenzi wa bwawa ambalo litahifadhi maji kipindi chote cha msimu wa kilimo.

Alisema ujenzi wa bwawa hilo utasaidia kilimo cha mpunga kulimwa muda wote na kuleta tija, kwa sababu mkulima atakuwa na uhakika wa maisha na kumudu gharama.

"Serikali imetusaidia kuboresha miundombinu ya umwagiliaji kwa kutujengea bwawa na sasa wakulima wetu watalima kipindi chote cha mwaka tunakoelekea wilaya yetu itakuwa ndio kitovu wa kuzalisha mpunga hapa nchini," alisema Mwambasa.

Miongoni mwa wakulima hao, akiwamo Emily Lubala, alisema kipindi cha nyuma walikuwa wanategemea mvua, lakini ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji na ujenzi wa bwawa, umewasaidia kuongeza mavuno.

Naye mfanyabiashara wa zao hilo, Nicolaus Nkya, alisema baada ya serikali kuboresha Skimu ya Naming'ongo, wanapata mazao mengi kwa muda mfupi wanaponunua tofauti na miaka ya nyuma kabla ya kujengwa daraja na kuboreshwa miundombinu eneo hilo.

# RC Chalamila ataka sheria ukusanyaji mapato isimamiwe

**Na Grace Mwakalinga,** KYELA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, ameutaka uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela kusimamia sheria za ukusanyaji mapato na ushuru na kuupuza watu wanaotumia mwanya wa ofa ya Rais Dk. John Magufuli kusafirisha mazao bure bila kulipa ushuru.

Alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki akiwa wilayani Kyela baada ya kusema kumezuka tabia ya baadhi ya wafanyabiashara kusafirisha mazao yanayozidi tani moja na wanapohojiwa wanadai Rais Magufuli aliruhusu mazao kusafirishwa bure.

Alisema endapo hali hiyo itavumiliwa kuna uwezakano mkubwa wa halmashauri na wilaya za mkoa huo kupoteza mapato na badala yake wasimamie kanuni na sheria za ukusanyaji mapato na ushuru.

"Lazima tusimamie sheria, Rais alikuwa na nia njema ya kuwasaidia wakulima pamoja na wafanyabiashara, ninachowaomba viongozi wenzangu simamieni sheria hasa kwa hawa wafanyabiashara, yeyote atayesafirisha mazao lazima atozwe ushuru wa mazao hata kama atakuwa anasafirisha gunia mbili," alisema Chalamila.

Aliutaka uongozi wa wilaya kuwa na mshikamano baina ya madiwani na watendaji ili kuwezesha kutimiza malengo ya makusanyo waliyojiwekea na kwamba mwaka wa fedha 2019/2020 bado halmashauri hiyo imekusanya asilimia 60 ya malengo ya makusanyo.

Kwa mujibu wa taarifa kutoka Ofisi ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Halmashauri ya Wilaya ya Kyela imeendelea kupata hati inayoridhisha kwa mwaka wa tatu mfululizo.

**Lazima tusimamie sheria, Rais alikuwa na nia njema ya kuwasaidia wakulima pamoja na wafanyabiashara, ninachowaomba viongozi wenzangu simamieni sheria hasa kwa hawa wafanyabiashara, yeyote atayesafirisha mazao lazima atozwe ushuru wa mazao hata kama atakuwa anasafirisha gunia mbili**





# Mwani kuanza kuzalisha chakula cha kuku

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Kilimo Maliasili na Mifugo ipo katika hatua za mwisho za kuzalisha chakula cha kuku ambacho kinatokana na malighafi ya zao la mwani.

Waziri wa Wizara hiyo, Mmanga Mjengo Mjawiri, alisema hiyo ni sehemu ya kuongeza thamani ya zao la mwani kwa ajili ya kuwapatia wakulima faida kubwa.

Akizungumza katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, waziri huyo alisema utafiti unaonyesha kwamba chakula cha kuku kinachozalishwa kutokana na kusarifiwa kwa zao la mwani ni borana chenye lishe nzuri ambacho husaidia mifugo hiyo kuhimili na maradhi mbalimbali.

"Napenda kuwajulisha wafugaji pamoja na wakulima wa zao la mwani kwamba tupo katika hatua ya mwisho ya kuzalisha chakula cha kuku kinachotokana na kusarifiwa kwa zao la mwani," alisema.

Alisema hizo ni habari nzuri kwa wakulima wa zao la mwani ambao sasa wanayo nafasi kubwa ya kuongeza juhudi za uzalishaji wa zao hilo kwa njia ya kisasa na kuleta tija.

Alieleza kuwa wakulima wa mwani sasa wanatakiwa kulima kilimo hicho katika maji yenye kina kirefu kufuatia kujitokeza kwa mabadiliko ya tabianchi ambapo mwani hunyauka na kufa.

"Zipo taarifa kwamba mwani mwingi umeathirika na kupata na maradhi mbalimbali kwa sababu ya joto na mabadiliko ya tabianchi ambapo mwani hupata maradhi na kunyauka," alisema.

Aliwataka wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wanaotoka katika majimbo yanayolimwa zao la mwani kuwahamasisha wakulima ambao wengi ni kinamama kuongeza kasi ya kilimo hicho ili kuimarika kiuchumi.

Alisema mashine hiyo itakuwa na uwezo wa kuzalisha chakula cha kuku jumla ya tani 50 kwa siku, na kuwataka wafugaji kujitayarisha kukitumia chakula hicho kwa ajili ya kuimarisha mifugo.



Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi, Mgeni Hassan Juma (kulia), akizungumza na Mwakilishi wa Jimbo la Bubwini, Mtumwa Peya, nje ya ukumbi wa baraza hilo, Chukwani Zanzibar jana. .**PICHA|: RAHMA SULEIMAN, ZANZIBAR**

# Viongozi waaswa ubaguzi wa dini, kabila

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

VIONGOZI wa taasisi mbalimbali katika Mkoa wa Kusini Unguja wametakiwa kuwahudumia wananchi bila kuwapo na ubaguzi wa dini wala kabila.

Mkuu wa Mkoa huo, Ayoub Muhamed Mahmoud, alisema endapo viongozi watafuata maadili na misingi iliyowekwa na serikali, itaweza kuwafanya waondokane na ubaguzi katika kutekeleza majukumu yao hali itakayopelekea imani kubwa kwa jamii wanayoiongoza.

Ayoub aliyasema hayo alipokuwa akizungumza na waumini wa dini ya Kikristo katika Kanisa Katoliki Parokia ya Mtakatifu Anthony wa Padua lililopo Machui Mkoa wa Kusini Unguja, kwenye Ibada ya Misa ya Utatu Mtakatifu.

Alisema serikali iliyopo madarakani haina dini, hivyo inatoa haki na usawa kwa wananchi wake kwa kuwapa huduma wanazostahiki bila ya ubaguzi.

"Serikali ya Zanzibar itaendelea kusimamia imani za waumini wote na kuwapatia huduma muhimu zinazostahiki kwa maendeleo ya Taifa," alisema.

Aidha, alisema serikali inatambua umuhimu wa kuabudu licha ya kutokuwa na dini, hivyo itasimamia usalama wao wakati wa kuabudu na kuendelea kutunza amani na utulivu uliopo.

Alieleza kuwa serikali inatambua michango inayotolewa na viongozi wa madhehebu mbalimbali yaliyopo nchini kwa kuwaelimisha na kuwafundisha waumini wao mambo mema na kuwakataza mabaya, hali inayopelekea kuwa ustawi mzuri wa jamii na vizazi vyenye tabia njema.

Alisema ni vyema kuona madhehebu yote nchini yanatekeleza majukumu yake bila ubaguzi sambamba na kuwapatia waumini wao elimu ya afya na ya kujikinga na virusi vya corona, kwani bado vipo licha ya kupungua kwa kiasi kikubwa.

Naye Paroko wa Kanisa hilo, Padre, Raphael Ramdinzalalila, aliwataka waumini wa dini ya Kikristo nchini kuendelea kudumisha ushirikiano, umoja na kutunza amani na utulivu uliopo nchini.

Aliwasihi waumini hao na wananchi kwa ujumla kufuata maelekezo mbalimbali yanayotolewa na serikali na kufuata sheria za nchi na kuendelea kuchukua tahadhari dhidi ya maambukizo ya virusi vya corona.

# Waziri avutiwa vita vya malaria

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

NAIBU Waziri wa Afya, Harusi Said Suleiman, ameitaka jamii kuthamini juhudi zinazochukuliwa na serikali katika kujikinga na malaria kwa kutumia vyandarua vilivyotiwa dawa.

Hayo aliyasema katika Shehia ya Sogea Wilaya ya Mjini Unguja, alipokuwa akizindua ugawaji wa vyandarua vilivyotiwa dawa vikiwa na lengo la kujikinga na malaria kwa wananchi katika baadhi ya shehia zenye maambukizo.

Alisema Wizara ya Afya ikishirikiana na Serikali za Wilaya itaendesha zoezi la ugawaji wa vyandarua vilivyotiwa dawa katika baadhi ya shehia ambazo zinaonekana bado zina maambukizo katika Wilaya ya Mjini, Magharibi 'A' na Magharibi 'B' Unguja.

Hivyo aliwaomba wananchi kuvitumia vyandarua hivyo kwa lengo la kujikinga na malaria na kuacha tabia ya kuvitumia kwa mambo mengine ikiwamo kuvifanya uzio katika bustani za mboga.

"Tuna wajibu wa kuthamini juhudi za serikali zinazofanywa kwa wananchi wake ili wawe na afya bora na kutokomeza kabisa maradhi ya malaria kwani iwapo tutakuwa na mashirikiano na kufuata miongozo inayotolewa na Wizara ya Afya Zanzibar bila ya malaria inawezekana," alisema Naibu wa Afya.

Alisema wananchi katika shehia nyingine wataendelea kupata vyandarua kwa utaratibu wa kuchukua kuponi kwa masheha wao na kwenda katika vituo vyao vya afya kupatiwa vyandarua.

Alieleza kuwa wagawaji wa vyandarua watazingatia taratibu zote za kujikinga na ugonjwa wa corona wakati wa zoezi hilo kwa kuvaa barakoa, kutumia vitakasa mikono pamoja na kuvaa glovu wakati wote.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Mjini Unguja, Marina Joel Thomas, aliwaomba masheha kuhakikisha vyandarua hivyo vinawafikia walengwa kwa mpango uliyowekwa, na kuwataka wananchi kuvitumia vyandarua hivyo kama vilivyokusudiwa na serikali.

Kwa upande wake Mkurugenzi Kinga na Elimu ya Afya, Dk. Fadhil Mohammed, aliwataka wananchi kufuata miongozo ya Wizara ya Afya kwa kuweka mazingira safi ili kuepuka mbu wasizaliane.

Naye Sheha wa Shehia ya Sogea, Abdullah Mohamed Abdullah na Diwani Mohamed Said Mohamed, walisema watahakikisha wananchi wanavitumia vyandarua hivyo kujikinga na ugonjwa wa malaria.

Jumla ya vyandarua 197,000 vitagawiwa kwa kaya 90,000 za wilaya zote tatu katika shehia 52 zikiwamo shehia 32 Wilaya ya Mjini, shehia 10 Wilaya ya Magharibi 'A' na Shehia 10 Wilaya ya Magharibi 'B' Unguja.

# TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**NAFASI ZA KAZI**

**NAFASI ZA KAZI YA DEREVA NA MAUZO** Mwenye uzoefu wa kuuza Maji. PIga simu namba : **0767 269677 saa za kazi**


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

**Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676**


## KUPOTEA KWA VYETI



**VERONICA KISHA** anatangaza kupotelewa na vyeti,cheti cha kidato cha nne **index No S.2453/0047** kilichotolewa na shule ya sekondari MPUI mwaka 2016, result slip ya kidato cha sita **index No. P4512-0517** NIA OPEN SCHOOL mwaka 2019 .Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo chochote na polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/416817/2020.**

115766002

## KUPOTEA KWA VYETI



**MHOJA ANDREA MBUSHI** anatangaza kupotelewa na vyeti vya kidato cha nne, shule ya sekondari Tumaini chenye **Index NO,0348-0024** kilichotolewa mwaka 1999. Cheti cha Tanganyika Medical Training Board **No, 9876,** cheti cha Uuguzi chenye **No 38843,** Cheti cha Ukunga chenye No 29993 vyote vilivyotolewa mwaka 2010 na chuo cha uuguzi Geita School of Nursing. Yeyote atakaye viona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **MAJ/RB/4718/2020.**

115765701

## KUPOTEA KWA CHETI



**ISIHAKA S. SAIDI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S3607.0020** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia MTOPWA SEKONDARI mwaka 2015. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **SO/RB/1334/2020.**

115766202

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Ndugu, **YOHANA KANURA** SAMWEL anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T- 714 CVE,** chasis namba **NT 30074087** aina ya **NISSAN X TRAIL.** kwa atakae iona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo karibu kwa **KUMB: NY/RB/434006/2020.**

115766102

**JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455.
Fax: +255 26 2323233.
Barua Pepe: ps@mow.go.TZ.
Tovuti: www.mwtc.go.TZ.

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470DODOMA
08/06/2020

## TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **JUMATANO tarehe 10/06/2020** kampuni ya **CIVIL LOTHS ENTERPRISES LTD** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa. Kutoka **SONGEA kuelekea DAR ES SALAAM,** Gari hilo yana namba za usajili: **T 735 DRM/ T 295 DRG**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita** | **17.80** |
| **Upana** | - | **mita** | **3.0** |
| **Kimo** | - | **mita** | **4.6** |

3. Njia itakayotumika: **SONGEA hadi DAR** kupitia **MIKUMI** Gari litasafiri muda wa mchana tu ***(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**JOHN JOSEPH KISHIWA** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba **T 479 CNV** aina ya SANLG yenye Chassis namba **LBRCPJB** 58D9024532. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo karibu yake.Taarifa ya Polisi. **KAH/TR/RB/08/2020.**

115765802

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KTK MAHAKAMA YA MWANZO MJINI ILIYOPO MOROGORO**

**TANGAZO LA KUITWA SHAURINI**

**SHAURI LA MADAI NAMBA:36..2020**

**Mdai.......................................PIENCIA NKEZA**

**DHIDI YA**

**Mdaiwa................EBRANIA PASCHAL MHIMBA**

**Kwa:**
**EBRANIA PASCHAL MHIMBA**

**Ombi la Mdai: PIENCIA NKEZA**
**Madai ya: TARAKA NA MGAWANYO WA MALI**

Unatakiwa kuudhuria hapa mahakamani ktk shauri tajwa hapo juu bila kukosa.Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 12 mwezi 06 mwaka 2020 saa 02:30 Asubuhi.
Angalia kama hukuudhuria/hamkuudhuria siku iliyotajwa hapo juu.Mahakama ikidhibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini,hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa /mmeshindwa.
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 03 mwezi 06 mwaka 2020.




115767002

## MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na **TUJIJENGE TANZANIA LTD, KATEMANA AUCTION MART** tutauza kwa mnada wa hadhara nyumba ya mdaiwa sugu iliyopo **Mtaa wa Mwembeni – Nyankumbu (GEITA), mali ya Ndugu Hismah Idd Said. Mnada utafanyika tarehe 20/06/2020 kuanzia saa nne asubuhi, mahali dhamana ya nyumba ilipo.**

Lengo ni kufidia / kupunguza deni la mkopo analodaiwa.

Mteja atalipa 25% siku ya mnada, 75% atalipa ndani ya siku 14 akishindwa kulipa 25% hairudishwi. Gharama za kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.

**Kwa Mawasiliano piga:-**
**0713408835 /0784988615 /0763452525**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo**

**MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;145/2020**

**Ombi la PASCHAL JOHN MNEMWA**
**Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu BLANDINA JOHN NJEGA.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 08/07/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 08/06/2020.




115766502


*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Tupigie 0782253676*


## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**KICHANGANI INVESTMENT CO LIMITED** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya **TVS STAR** yenye namba za usajili **MC 705 CGB.** Chassis **No.MD625AF75K1AL1273,** Engine **No.AF7AK15L1710.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/375123/2020.**

115765902


**Uza, Chenye Thamani Kubwa**

**Kwa Kutangaza Nasi**

**Kwa Bei Poa**

**Tupigie 0782253676**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Sababu tano Bunge kumpongeza Ndugai

**Na Sanula Athanas, DODOMA**

BUNGE limepitisha azimio la kumpongeza Job Ndugai, Spika wa Bunge la Tanzania kwa kuliwezesha Bunge la 11 kupata mafanikio, likianika mambo matano makuu yaliyofanyika.

Akiwasilisha hoja hiyo jana, Mbunge wa Misungwi, Charles Kitwanga (CCM), alitaja mambo matano yaliyofanywa katika kipindi cha Bunge la 11 kuwa ni pamoja na kubuni wazo la Bunge Mtandao (e-Parliament).

Alisema utandawazi wa Bunge Mtandao umewawezesha wabunge kupata vishikwambi (tablets) ambavyo wanatumia katika shughuli mbalimbali za kibunge huku Ofisi ya Bunge ikitarajia kuokoa zaidi Sh. bilioni nne kwa mwaka baada ya kuanza kutumia Bunge Mtandao.

Pia, imeelezwa kwamba inakadiriwa kuwa zaidi ya Sh. bilioni 100 zinatarajiwa kuokolewa kutoka kwenye matumizi ya wizara na taasisi mbalimbali za serikali kutokana na matumizi ya Bunge Mtandao ambapo sasa wizara na taasisi za serikali zimepunguza matumizi ya karatasi kwa zaidi ya asilimia 90.

Alisema jambo la pili ni kupunguza matumizi yasiyo ya lazima, akieleza kuwa Bunge lilikubali kumuunga mkono Rais kwa kubana matumizi yake kwa kupunguza matumizi yasiyo ya lazima kama vile kupunguza safari zisizo za lazima nje ya nchi.

Alisema amefanya utafiti mdogo na kubaini kuwa bajeti ya mwisho ya Bunge la 10 (2015/2016) ilikuwa takribani Sh. bilioni 173.77 wakati bajeti ya mwisho ya Bunge la 11 (2020/2021) ni Sh. bilioni 121.79.

Alilitaja jambo la tatu kuwa ni kuongezeka kwa ofisi na kumbi za mikutano, lililosaidia kuondoa kabisa gharama ambazo zilikuwa zinatumika kukodi kumbi za mikutano wakati wa vikao vya kamati.

Alisema inakadiriwa kuwa zaidi ya Sh. milioni 120 kila mwaka sawa na Sh. milioni 600 kwa miaka mitano zimeokolewa baada ya Bunge kuanza kutumia kumbi zilizoko katika majengo yake.

Jambo la nne ni maboresho ya miundombinu, akieleza kuwa wabunge wanajivunia maboresho ya miundombinu mbalimbali ya Ofisi ya Bunge.

Jambo la tano kuwa ni kulinda hadhi, staha na taswira ya Bunge. Alisema Bunge la 11 ndiyo Bunge lenye idadi kubwa ya wabunge vijana na wabunge kutoka vyama vya upinzani kuliko kipindi chochote cha historia ya nchi.

# Waziri asweka ndani viongozi kijijini madai kuhujumu maji

**Na Mwandishi Wetu, KIBAKWE**

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, amewaagiza Polisi kumkamata Mwenyekiti, Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Chogola, Jimbo la Kibakwe na mafundi bomba wawili wa Wakala ya Usambazaji Maji na Usafi na Mazingira Vijijini (RUWASA) wilayani Mpwapwa kwa kosa la kuhujumu mradi wa maji wa kijiji hicho.

Mamia ya wakazi wa kijiji hicho ambao walikuwa na hasira ya kukosa maji kwa muda mrefu, walimlalamikia waziri huyo, wakidai maji ambayo yalikuwa yanatoka kwa wingi kijijini hapo, lakini kwa sasa hayatoki kutokana na viongozi wao wa kijiji kuhujumu mradi huo wa miaka mingi.

Akizungumza na wananchi wa kijiji hicho, Kata ya Chogola, Waziri Simbachawene, alisema viongozi hao ambao walikuwapo katika mkutano huo wanapaswa kufikishwa kwenye vyombo vya sheria haraka iwezekanavyo kutokana na kushindwa kutekeleza majukumu yao pamoja kuhujumu mradi huo.

Alisema amefanya ukaguzi wa mradi huo na kupata maelezo ya kutosha kutoka kwa wananchi, viongozi wa vijiji pamoja na Ruwasa, kuwa 'air valve' ya bomba kuu la maji ambayo yanasambaza kijiji hicho imeondolewa na haijulikani ilipo na pia mabomba ya chuma yameondolewa na kuwekwa ya plastiki.

"Valve ya bomba la maji iliyokuwapo katika mradi huu ni ya mwaka 1973, ambayo mradi huo ulikamilika, lakini wananchi wanalalamika kuwa valve ya mwaka 1973 haipo imeondolwa na haijulikani ilipo, hivyo ikawekwa ya mwaka 1974 ambayo sio imara na makosa yamefanyika," alisema na kuongeza:

"Tunataka hiyo valve irudi hata kama imechakaa, na ikiapatikana iwekwe katika ofisi ya kijiji na wananchi waione."

Pia alisema mabomba ambayo yapo katika mradi huo yameondolewa na mafundi bila taarifa ya uongozi wa kijiji, hivyo kusababisha maji kutotoka vizuri na muda mwingine kutokuwapo kabisa.

"Polisi pia muwakamate mafundi bomba wa mradi huu, wamesababisha kuwapo kwa matatizo haya makubwa na mamia ya wananchi wanalalamika ukosefu wa maji kijijini hapa, kwanini walibadilisha mabomba haya na bila taarifa ya uongozi wa kijiji, hii sio sahihi, wanapaswa kukamatwa na kupelekwa, polisi wasakate popote walipo mafundi hao," alisema Simbachawene.

Baada ya maagizo hayo, Simbachawene aliwataka wananchi wasizuie mradi huo kukarabatiwa na Ruwasa, na pia Meneja wa Mradi huo kutoka Ruwasa, Mhandisi, Cyprian Warioba hana kosa hivyo wanakijiji wamlinde wakati anaendelea kufanikisha maji yanarudi katika hali yake ya awali kijijini hapo.

"Mhandisi wa mradi huu hana kosa, mpeni ushirikiano aendelee na kazi yake, msizuie mradi huu, acheni uendelee, pia mhandisi wa mradi nakuagiza hakikisha leo maji yanapatikana hapa kijijini, mabomba yote ya chuma yanarudi na kuyaondoa haya ya plastiki mliyoyaweka, na pia nakupa wiki tatu mradi huu ukamilike nije kuufungua hapa kijijini," alisema Simbachawene.

Aidha, Waziri Simbachene alisema amezungumza na Waziri wa Maji ana amesema mradi huo umetengewa shilingi milioni 154, na tayari shilingi milioni 60 zilishatolewa kwa Ruwasa ili mradi huo uweze kukamilika na wananchi hao wananufaika kwa kupata maji.

Waziri Simbachawene aliwasili kijijini hapo baada ya siku moja kabla ya kuzuiwa na wananchi hao wakimwomba kumsaidia kupata maji ambayo yamehujumiwa na viongozi wa kijiji hao pamoja na wafanyakazi wa Ruwasa.

Meneja wa Mradi huo, Mhandisi Cyprian Warioba, alimhakikishia waziri huyo maji yatapatikana kijijini hapo kwa siku hiyo hiyo aliyoagiza, na pia maelekezo aliyoyatoa atayafanyia kazi.

Hata hivyo, baada ya ukaguzi wa mabomba hayo alibaini kuwa kuna mgogoro baina ya wananchi na viongozi wa kijiji hicho kwa kubadilisha valve pamoja na kungo'a bomba za maji hali ambayo imepelekea wakazi wa kijiji hicho kutopata maji kwa muda mrefu.

Viongozi wa vijiji waliokamatwa ni Mwenyekiti wa Kijiji, James Kisagase na Mtendaji wa Kijiji, David Msumuche pamoja na mafundi wa bomba wa Ruwasa ambao walikuwa bado wanatafutwa na polisi.



Mchungaji wa Kanisa la Christ Embassy la Mbezi, jijini Dar es Salaam, Ken Igini (kulia), akikabidhi kwa niaba ya Mchungaji Chris Oyakhilome, msaada wa chakula chenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 4, kwa Mchungaji wa kanisa la Pentekoste Lugoba, Martini Machana, aliyepokea kwa niaba ya wachungaji wanzake wa kanisa hilo, Chalinze, mkoa Pwani mwishoni wa wiki, ili kujikimu katika kipindi hiki cha janga la corona. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Benki CBA, NIC kuungana

**Na Mary Mshami, UDOM**

BENKI ya Afrika (CBA) na NIC zinatarajia kuungana na kujulikana kama NCBA kuanzia Julai 8, mwaka huu, kwa ajili ya kuimarisha uchumi na muunganiko wa kibiashara.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwenye gazeti la The Guardian, na kusainiwa na Meneja Masoko wa Benki ya Afrika, Gift Shoko, muunganiko huo hautaathiri wateja wao.

"Wasiwe na hofu juu ya muunganiko huo hii yote ni kuimarisha biashara na kujenga uhusiano mzuri baina ya hizo benki mbili, muunganiko huu umetokana na makubaliano ya pande zote mbili za benki kuleta ushindani mzuri," alisema.

Pia, benki hizo zipo katika mchakato wa kutengeneza sifa na sheria ambazo zitakidhi vigezo na kumwezesha mteja kufurahia huduma mpya.

"Muungano wa benki hizi mbili unatarajiwa kufanyika kwa siku 30 kuanzia jana hii, ni mara ya kwanza kwa benki hizi kuungana nchini, wateja wanaombwa wawe na uvumilivu kwa mabadiliko haya yanayojitokeza kwa siku chache kwa ajili ya kuboresha huduma," alisema.

# COURTOIS:
## REAL MADRID INAMHITAJI SANA HAZARD




**MADRID, Hispania**

GOLIKIPA wa Real Madrid, Thibaut Courtois amesema 'Los Blancos' hao watamhitaji Eden Hazard kwa ajili ya kuwania ubingwa wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, msimu huu.

Hazard amecheza mechi 15 kwa Madrid tangu alipotua hapo akitokea Chelsea kwa ada ya euro milioni 100 kutokana na majeraha ya mara kwa mara.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, alivunjika kifundo cha mguu kabla ya msimu wa LaLiga kusimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona, lakini ametumia karibia miezi mitatu kujiuguza na sasa ana nafasi ya kurudi uwanjani baada ya kupona kabisa kabla ya ligi kurudi.

Madrid - ambao wamepitwa pointi mbili na vinara wa ligi hiyo, Barcelona huku zikiwa zimebaki mechi 11 ligi hiyo kumalizika msimu huu, wataanza na Eibar Juni 14 na Courtois ameelezea maendeleo ya mchezaji mwenzake, Hazard.

"Hazard yuko fiti," alisema mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji, Courtois akiambia Movistar. "Anaonekana kurudi kwenye kiwango chake, lakini atalazimika kwenda taratibu.

"Hatuwezi kumtarajia kuwa kwenye kiwango cha juu bila kucheza. Nafikiri yupo kwenye wakati mzuri na tutamhitaji yeye kwa ajili ya kupambana kuwania taji."

Madrid ilishinda mchezo mmoja tu kati ya mechi nne zilizopita za LaLiga kabla ya msimu kusimama kutokana na ugonjwa wa Covid-19, Machi mwaka huu.

Kikosi hicho cha kocha, Zinedine Zidane kiliwafunga wapinzani wao Barca kwa mabao 2-0 Machi, mwaka huu lakini wakafungwa na Real Betis na Levante, huku wakitoka sare nyumbani kwa Celta Vigo.

"Tunasubiri kuanza kwa ligi na kuanza kupambana ili kubeba taji," alisema Courtois wakati Madrid wakijiandaa kucheza bila mashabiki uwanjani.

"Itakuwa ni tofauti kucheza bila mashabiki uwanjani," aliongeza kusema Courtois.



## MBAPPE ATABIRIWA UFALME LIVERPOOL

**PARIS, Ufaransa**

KYLIAN Mbappe atakuwa "Mfalme" kwa Liverpool chini Jurgen Klopp na kwamba, klabu hiyo inafiti aina yake ya uchezaji, kwa mujibu wa mchezaji wa zamani wa Ufaransa, Willy Sagnol.

Sagnol amesema litakuwa ni chaguo sahihi kwa mshindi huyo wa Kombe la Dunia, Mbappe, kutua Liverpool.

Uhamisho wa kutua Anfield umekuwa ukizungumziwa kwa straika huyo mwenye umri wa miaka 21, ambaye bado ni mchezaji wa Paris Saint-Germain.

Mafanikio waliyoyapata Liverpool ndani ya miezi 12 pamoja na uwapo wa Klopp katika benchi la ufundi, vinafanya klabu hiyo kuwa mahali sahihi kwa kipaji hicho kikubwa zaidi duniani.

Sagnol anaamini Liverpool itafiti vema kwa Mfaransa mwenzake huyo, na kwamba kuna kila sababu soka la Mbappe likaongezeka ubora.

"Klabu ya Liverpool itakuwa na faida kubwa sana kwake," alisema Sagnol akinukuliwa na gazeti la Bild la Ujerumani.

"Ukiwa na Klopp una kocha ambaye kila mchezaji duniani anatamani kufanya kazi naye.

"Mbappe atahitaji kubadilika chini yake. Anahitaji washambuliaji wake wafanye kazi kubwa kusaidia ulinzi, jambo ambalo Mbappe hayuko vema.

"Lakini anaweza kujifunza hilo, hasa kwa mtu kama Klopp. Hamna maswali. Mbappe anaweza kuwa mfalme chini ya Jurgen Klopp pale Liverpool."

# Fernandes kalia kusajiliwa United

**MANCHESTER, England**

IMEBAINISHWA kwamba, Bruno Fernandes alimwaga machozi alipoambiwa kuhusu uwezekano wa kujiunga na klabu ya Manchester United.

Kiungo huyo raia wa Ureno alijiunga rasmi na 'Mashetani Wekundu' hao akitokea Sporting Lisbon Januari baada ya kuhusishwa mfululizo na uhamisho huo mwaka mmoja uliopita.

Akiwa amekua akimwona Cristiano Ronaldo akitengeneza jina lake kwenye Ligi Kuu ya England akiitumikia Man United, Fernandes amebainisha kuwa alipagawa kusikia ndoto yake inaelekea kuwa kweli.

"Unajua, nitasema ukweli niliogopa," Fernandes alisema kupitia mahojiano ya Instagram mubashara aliyofanyiwa na Mario Djurovski. "Ilikuwa ni ndoto iliyokuja kuwa kweli.

"Kwangu mimi kucheza soka England na kuitumikia Manchester United ilikuwa ni ndoto ya juu kabisa katika maisha yangu ya soka. Kucheza kwenye Ligi Kuu ya England katika moja ya timu bora duniani.

"Nilipopokea simu ikisema: 'Bruno, una nafasi ya kuhamia Manchester' nilimpigia mke wangu, kaka yangu, dada yangu, mama yangu na kuanza kulia.

"Lakini nilikuwa nalia kwa furaha. Nimepambana kwa maisha yangu yote ili kufikia jambo hili, kuchezea klabu hii. Nafasi ilikuwa pale na nilitaka kuikamata kwa mikono yangu yote miwili, kuifuata ndoto yangu."

## HABARI MICHEZO




# MESSI

## NI BORA ZAIDI DUNIANI – DE JONG

**BARCELONA, Hispania**

LIONEL Messi “ni mchezaji bora duniani,” kwa mujibu wa mchezaji mwenzake wa Barcelona, Frenkie de Jong.

Messi anachukuliwa kama mmoja wa wachezaji bora zaidi wakati akitamba kwenye Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga akiwa na miamba Barca, huku mshambuliaji wa Juventus, Cristiano Ronaldo pia akitajwa kuwa bora.

Mshindi huyo mara sita wa tuzo ya Mchezaji Bora wa Dunia [‘Ballon d’Or’], Messi ameshinda mataji ya LaLiga mara 10 na manne ya Ligi ya Mabingwa Ulaya tangu alipoanza kuichezea Barca mwaka 2004.

Na De Jong mchezaji wa kimataifa wa Uholanzi, amemsifia Messi mwenye umri wa miaka 32 kuelea kurudi kwa msimu wa LaLiga baada ya mlipuko wa virusi vya corona.

“Kama Messi anazungumza na kukupa ushauri, unauchukua kwa sababu yeye ni mchezaji bora duniani. Kama akikupa ushauri, unasikiliza,” alisema De Jong akiiambia BBC Radio 5 Live.

Barca inaongoza msimamo wa LaLiga kwa pointi mbili zaidi kileleni dhidi ya wapinzani wao Barca, huku zikiwa zimebaki mechi 11 msimu kumalizika na itaanza na Real Mallorca Juni 13.

## Sterling apigana na ubaguzi wa rangi

**MANCHESTER, England**

RAHEEM Sterling amesema kwa sasa dunia inasumbuliwa na ugonjwa pekee wa ubaguzi wa rangi.

Winga huyo wa Manchester City na timu ya Taifa ya England, ambaye ni moja wa waathirika wa ubaguzi wa rangi amebainisha kwamba, jambo hilo limekuwa wimbo kwa kila taifa.

Sterling mwenye umri wa miaka 25, amesema ataendelea kuzungumza kila wakati ubaya wa ubaguzi wa rangi mpaka pale utakapofika kikomo.

Alisema watu kwa sasa wapo tayari kwa mabadiliko ndio maana kila eneo wanapambana kuona hali inakuwa salama na wote wakaishi kwa usawa.

Kwa sasa watu wengi wakiongozwa na wale wa Marekani wameonekana wakiandamana kwa amani kupinga kuuawa kwa George Floyd mwenye miaka 46, ambaye alikufa mikononi mwa Polisi wa Marekani Mei 25.

“Najua ni lazima hali kama hiyo itokee, ukweli ni kwamba kwa sasa dunia inapambana na ugonjwa mmoja tu ambao ni ubaguzi na imekuwa ikitokea miaka na miaka. Tunahitaji kutafuta njia ili kusimamisha haya,” alisema.




# Van de Sar athibitisha Utd kumtaka De Beek

**AMSTERDAM, Uholanzi**

MKURUGENZI wa Michezo wa Klabu ya Ajax, Edwin van der Sar amethibitisha kwamba Manchester United imeonyesha nia ya kutaka saini ya nyota wao, Donny van de Beek.

Van de Sar ambaye alikuwa golikipa wa United kati ya mwaka 2005 na 2011 kabla ya kurudi katika klabu yake hiyo ya zamani, amebainisha kwamba, Real Madrid pia inamtaka mchezaji huyo.

Akinukuliwa na NOS, Van der Sar alisema: “Ipo wazi kabisa kuna timu ambazo zinamhitaji Donny van de Beek - Manchester United na Real Madrid.”

Madrid walikuwa wakitajwa kuitaka saini ya kiungo huyo muda mrefu ila janga la virusi vya corona lilitibua mipango ya mazungumzo yao.

Nyota huyo mwenye miaka 23, amekuwa msaada mkubwa ndani ya Ajax jambo lililozivutia timu nyingi.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# DYBALA: NIMEPONA CORONA LAKINI SIKO FITI

●●●Sijawa fiti kwa asilimia 100, lakini niko vizuri, tumekuwa tukifanya mazoezi na ligi inarudi hivi...

**TURIN, Italia**

PAULO Dybala amebainisha kwamba bado hayuko fiti kwa asilimia 100 baada ya kupona virusi vya corona, lakini anafurahia kurudi kwenye Ligi Kuu ya Italia, Serie A.

Mshambuliaji huyo wa Juventus alithibitisha Machi mwaka huu kwamba amepata maambukizo ya corona yeye na mpenzi wake, Oriana Sabatini, wakati ambao soka la Italia lilisimamishwa kutokana na mlipuko huo.

Dybala alilazimika kujitenga kwa mwezi mmoja kabla ya Juve kutangaza kwamba amepimwa mara mbili na kukutwa hana tena virusi hivyo Mei 6.

Alipokwenda kwenye mchezo wa hisani wa nyota wa Tottenham, Dele Alli, mchezaji huyo raia wa Argentina alibainisha kwamba anasubiri kurejea kwa msimu huu 2019-20.

"Nilikuwa na corona, lakini kwa sasa najisikia vizuri," alisema Dybala wakati wa mahojiano kupitia mtandao wa kijamii wa Instagram.

"Bado siko fiti sana kwa asilimia 100, lakini niko vizuri. Tumekuwa tukifanya mazoezi na ligi inarudi hivi karibuni, hivyo tutakuwa na wakati wa kufanya kile tunachokipenda sana.

"Natumaini tunaweza kuwa na wakati mzuri wa kufurahia.

"Ninafikiri tutakuwa vizuri na tutakuwa na mechi nyingi mfululizo kabla ya ligi kumalizika."

## KWA UFUPI

**CITY YAJITOSA KWA CHILWELL**
KLABU ya Manchester City ipo tayari kushindana na Chelsea kumsajili mlinzi wa Leicester City na England, Ben Chilwell mwenye umri wa miaka 23. ***(Telegraph)***

**KOULIBALY KUITAJIRISHA NAPOLI**
NAPOLI haitapunguza bei ya pauni milioni 100 kwa mlinzi wao, Kalidou Koulibaly mwenye umri wa miaka 28 raia wa Senegal - ambaye amekuwa akihusishwa na Manchester United licha ya matatizo ya kifedha kutokana na mlipuko wa virusi vya corona. ***(Mirror)***

**UNITED, REAL KWA MARTINEZ**
KLABU za Manchester United na Real Madrid zinafuatilia kwa karibu hali ya usajili wa mshambuliaji wa Inter Milan, Lautaro Martinez mwenye umri wa miaka 22, baada ya mazungumzo ya uhamisho wake wa kwenda Barcelona kusimama. ***(Marca via Mirror)***

**RAKITIC AKOMAA BARCA**
KIUNGO wa kimataifa wa Croatia, Ivan Rakitic mwenye umri wa miaka 32, anataka kubakia Barcelona hadi mkataba wake utakapomalizika kipindi cha majira ya joto 2021, licha ya ripoti kudai kwamba ataondoka mapema. ***(Goal)***

**CAVANI AITAMANI LA LIGA**
KUNGO wa Paris St-Germain, Ander Herrera mwenye umri wa miaka 30, amesema mchezaji mwenzake raia wa Uruguay, Edinson Cavani, ambaye mkataba wake unamalizika kipindi hiki cha majira ya joto, anataka kucheza Ligi Kuu ya Hispania, La Liga. Cavani mwenye umri wa miaka 33, amekuwa akihusishwa na Atletico Madrid. ***(Diario As via Mail)***

**SPURS YAMPOTEZEA ZANIOLO**
KLABU ya Tottenham Hotspur imeachana na mpango wa kutaka kumsajili kiungo wa kimataifa wa Italia, Nicolo Zaniolo mwenye umri wa miaka 20, kwa sababu klabu yake ya AS Roma inataka pauni milioni 62 ili kumuachia. ***(Star)***

**ODSONNE KUFUNGWA CELTIC**
KOCHA Neil Lennon amesema Celtic wapo kwenye mazungumzo ya kumwongezea mkataba mchezaji, Odsonne Edouard mwenye umri wa miaka 22, ambaye amekuwa akihusishwa na Arsenal na Manchester United. ***(Mail)***

**PJANIC AITAKA BARCA**
KIUNGO wa Juventus raia wa Bosnia-Herzegovina, Miralem Pjanic mwenye umri wa miaka 30, amekataa ofa kutoka Chelsea na Paris St-Germain kwa sababu anataka kujiunga na Barcelona. ***(Marca)***

**ANGELINO KURUDI CITY**
MCHEZAJI wa Hispania, Angelino mwenye umri wa miaka 23, anapanga kurudi Manchester City baada ya mkataba wake wa mkopo kumalizika kule RB Leipzig na haiwezi kumsajili kwa pauni milioni 25. ***(Manchester Evening News)***

**BALLACK AMTAKA WERNER CHELSEA**
KIUNGO wa zamani wa Chelsea, Michael Ballack ameunga mkono usajili wa mshambuliaji wa kimataifa wa Ujerumani, Timo Werner kutoka RB Leipzig na anaamini nyota huyo mwenye umri wa miaka 24, atazoea haraka soka la Ligi Kuu ya England. ***(Sky Germany)***

**KINDA UNITED OGOMBEWA**
MLINZI wa Manchester United, Brandon Williams mwenye umri wa miaka 19 anagombaniwa na mawakala wawili ambao wanataka kumsajili. ***(Mirror)***

HABARI MICHEZO

# CHAMA: UBINGWA BARA, FA CUP MUHIMU SIMBA

**Na Mwandishi Wetu**

HUKU akianza mazoezi ya peke yake baada ya kutua jana nchini akitokea kwao Zambia, kiungo mnyumbulifu wa Simba, Clatous Chama amesema licha ya kutarajia ushindani mkubwa Ligi Kuu Bara na Kombe la FA, anaamini watapigana kiume kuweza kutwaa mataji hayo mawili makubwa nchini.

Chama aliyechelewa kujiunga na wenzake kambini kutokana na mipaka ya nchini kwao kufungwa hiyo ikiwa ni baada ya kuibuka mlipuko wa virusi vya corona (COVID-19), jana alianza mazoezi ya peke yake akiwa chini ya uangalizi wa Kocha wa Viungo wa klabu hiyo, Adel Zrane.

Akizungumzia kuhusu maoni yake kuelekea kuhitimisha mechi zao 10 za mwisho Ligi Kuu na Kombe la FA ambalo wamefika hatua ya robo fainali, Chama alisema ushindani utakuwa mkubwa baada ya ligi kurejea wiki hii, lakini ana uhakika Simba itaendeleza moto wake kama ilivyokuwa kabla ya ligi hiyo Machi 17, mwaka huu kutokana na janga la corona.

"Simba kama bingwa mtetezi lazima ijipange vizuri ili kutetea taji la ligi na kutwaa Kombe la FA.

"Tunajua ligi ikirejea ushindani lazima utakuwa mkubwa, lakini sisi kama mabingwa lazima tuhakikishe tunafanya kila linalowezekana kutetea taji na kuchukua Kombe la FA," alisema Chama.

Chama aliongeza kuwa mchezo wa robo fainali wa Kombe la FA dhidi ya Azam utakuwa mzuri ambao utapaswa kutazamwa na mashabiki wengi kutokana na ubora wa timu zote.

"Azam ni timu nzuri na mechi itakuwa ya ushindani mkubwa, lakini matumaini yetu ni kuhakikisha tunapita na kuingia nusu fainali," alisema.

Baada ya Chama kujiunga na wenzake kambini, mchezaji pekee wa Simba aliyebaki ambaye hajarejea nchini ni kiungo Sharaf Eldin Shiboub aliyekwama kwao Sudan baada ya mipaka ya nchi hiyo kuendelea kufungwa kutokana na janga la virusi vya corona.

MILIKI...



Kiungo wa Yanga, Mnyarwanda Haruna Niyonzima, akimiliki mpira dhidi ya beki wa KMC FC kwenye mechi ya kirafiki iliyopigwa Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam juzi na Yanga kukubali kipigo cha mabao 3-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Azam yakerwa na 'mwili wako wangu'

**Na Saada Akida**

MTENDAJI Mkuu wa Azam FC, Abdulkarim Amin 'Popat' ameeleza kukerwa na kauli ya "mwili wako wangu" inayotolewa na mashabiki, huku akieleza kama hawatakubali kubadilika, serikali inaweza kuchukua maamuzi magumu ya kuwafungia kuingia viwanjani kushuhudia mechi mubashara.

Popat amefikia hatua ya kutoa kauli hiyo kutokana na kukerwa na baadhi ya mashabiki waliohudhuria mechi ya kirafiki kati ya Azam FC na Transit Camp kwenye uwanja wao wa Chamazi kwa kutokuwa wasikivu kutokana na kutokubali kuchukua tahadhari ya kukaa mbalimbali (Social distance) kama ambavyo Wizara ya Afya inaagiza kwa wale wanaohudhuria viwanjani.

Alisema wamepokea barua kutoka wizara husika juu ya kushindwa kuchukua tahadhari, lakini wao walifanya hivyo kwa kuwataka mashabiki kuvaa barakoa pamoja na kupita katika mashine ya kutakasa mikono, ila wanapoingia ndani ya uwanja wanakuwa wakaidi kwa kukubali kukaa mbalimbali.

"Tatizo linakuja kwa mashabiki kutokubali kukaa mbalimbali ikiwa ni kuchukuwa tahadhari, ukiwaambia kaeni mbalimbali wanahoji 'mwili wako, mwili wangu?' Hivyo kutokana na ubishi wao tunapoelekea tunaweza kufungiwa mashabiki wasiingie uwanjani.

"Tumeshuhudia katika mchezo wetu wa kirafiki na Trans Camp, mashabiki wanawajibu vibaya watu wetu waliowekwa kwa ajili ya kutoa tahadhari kuhusu namna ya ukaaji uwanjani," alisema Popat.

Alisema kwa kauli za mashabiki kutochukua tahadhari kunaweza kusababisha serikali na mamlaka husika kuchukua maamuzi ya kufungia viwanja na kucheza bila ya mashabiki.

Alisema leo wanatarajia kucheza mechi ya kirafiki dhidi ya KMC FC, lakini kutokana na changamoto hiyo, wanaweza kucheza bila ya mashabiki.

## JKU yapata pigo Ligi Z'bar ikirejea

**Na Hawa Abdalla, ZANZIBAR.**

KATIBU Mkuu wa timu ya JKU, Sadu Ujudi, amesema tayari wachezaji wake wameingia kambini kujiandaa na mechi za Ligi Kuu Zanzibar zilizosalia kabla ya msimu huu wa 2019/2020 kumalizika.

Akizungumza na gazeti hili jana, alisema wanaendelea kujiandaa kumalizia msimu huu wa ligi hiyo, huku wachezaji wake tegemeo wakiwa katika mafunzo ya kijeshi, lakini wanatumai huenda wakawapata kabla ya ligi kumalizika.

Alisema katika michezo ya mwanzo watalazimika kuwatumia baadhi ya wachezaji kutoka Timu B, ili kukiongezea nguvu kikosi chao wakati wakisubiri nyota hao waliopo mafunzoni.

"Wachezaji wetu tegemeo ambao wengi wao ni kikosi cha kwanza wameenda 'depo' matumaini ya kuwapata yapo japo si kwa asilimia 100, lakini timu imejipanga kuhakikisha inafanya vizuri na hata kuhakikisha lengo la kunyakuwa ubingwa linatimia," alisema.

JKU ambayo inamilikiwa na Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar, ipo nafasi ya pili katika msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar ikiwa na alama 45, wakati huu ligi hiyo ikitarajiwa kurejea Juni 20, baada ya kusimama tangu Machi 17, mwaka huu kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

## Mgosi atangaza vita Ligi Kuu Wanawake

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Simba Queens, Mussa Hassan 'Mgosi' ametoa tahadhari kwa wapinzani wake kuwa wanakuja kivingine kuhakikisha wanashinda katika michezo yao mitatu, ili kuweza kutangazwa mabingwa Ligi Kuu Wanawake nchini.

Hivi karibuni serikali iliruhusu ligi za soka nchini kurejea; ambazo ni Ligi Kuu Bara, Kombe la FA, Ligi Daraja la Kwanza na la Pili pamoja na Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania ambayo inatarajiwa kuanza Juni 21, mwaka huu huku Simba Queens wakianzia ugenini dhidi ya Ruvuma Queens ya mkoani Ruvuma.

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam juzi, Mgosi alisema kikosi chake kipo tayari kwa ajili ya mchezo wao huo watakaocheza Juni 22 ugenini mkoani Ruvuma.

Alisema malengo yao ni kuhakikisha wanashinda mechi zao zote hasa michezo mitatu dhidi ya Ruvuma, JKT Queens na Yanga ambayo itaihakikishia ubingwa.

"Tumerejea na upepo wa 'kisulisuli', hatuachi mtu salama, kikosi kipo imara malengo yetu ni kushinda michezo mitatu ikiwamo kuwafunga Ruvu, Yanga na JKT nina uhakika wa kutwaa taji hilo," alisema Mgosi.

Simba Queens inashika nafasi ya pili katika msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 29 wakati JKT Queens iliyopo kileleni ikiwa michezo miwili mbele.

# Michezo

Jumanne Juni 9, 2020

Nipashe




## Dybala: Nimepona corona lakini siko fiti

HABARI UK 22

MSITU...



Mshambuliaji wa Simba, Meddie Kagere, akipiga hesabu ya kupasua msitu wa mabeki wa Transit Camp kwenye mchezo wa kirafiki uliopigwa jana, asubuhi, katika Uwanja wa Mo Simba Arena, Bunju nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam na Simba kushinda 4-2 kabla ya jioni kuifurusha KMC FC 3-1 kwenye dimba hilo. **PICHA: SIMBA**

# SIMBA: KMC CHEZEENI WATOTO LAKINI SIO SISI

●●●Yatoa dozi mbili kwa siku ikianza na Trans Camp 4-2 na kisha 3-1, upana wa kikosi waonekana...

**Na Mwandishi Wetu**

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu Bara na vinara wa ligi hiyo msimu huu, wameonyesha upana wa kikosi chao baada ya jana kucheza mechi mbili za kirafiki na kufanikiwa kugawa dozi kwenye mechi hizo zilizopigwa katika uwanja wao wa Mo Simba Arena uliopo Bunju jijini Dar es Salaam na kueleza "wachezee watoto sio sisi".

Simba ilianza kwa kutoa dozi ya mabao 4-2 asubuhi dhidi ya Transit Camp ya Ligi Daraja la Kwanza, wafungaji wakiwa winga Mkongomani Deo Kanda dakika ya tatu, kiungo Mbrazil Gerson Fraga (dk 15), beki Mbrazil Tairone Santos (dk 17) na straika Mnyarwanda Meddie Kagere akafunga hesabu dakika ya 46.

Kwa upande wa Transit Camp mabao yao mawili yalifungwa na Hamadi Habibu dakika ya 45 na Nisile Kisimba (dk 64).

Simba ambayo ipo kwenye maandalizi ya Ligi Kuu Bara inayotarajiwa kurejea Jumamosi wiki hii kwa Yanga kuifuata Mwadui FC ya Shinyanga ikiwa ni siku moja kabla ya 'Wekundu wa Msimbazi' hao kuikaribisha Ruvu Shooting katika Uwanja wa Taifa, wachezaji wake walionyesha kuimarika kwa upande wa utimamu wa mwili ukilinganisha na watani zao wakati wakichezea kichapo cha mabao 3-0 dhidi KMC juzi katika Uwanja wa Uhuru.

Katika mechi ya jioni, Simba inayoongoza kwenye msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na alama 71, wakati huu ikibakiza mechi 10 kabla ya Ligi Kuu msimu huu kumalizika, ilikuwa ya kwanza kukubali kutobolewa baada ya KMC kupata bao la kuongoza kupitia kwa Charles Ilanfya aliyetupia dakika ya 30 ya mchezo huo uliohudhuriwa na mashabiki kibao ambao waliuzunguka uwanja.

Hata hivyo, iliichukua dakika nne tu tangu kuingia kwa bao hilo kwa Simba kuweza kusawazisha kupitia kwa nahodha wao, John Bocco 'Adebayor' ambaye alimtesa vilivyo mlinda mlango wa KMC aliyekuwa mchungu kwa Yanga juzi.

Timu hizo zilikwenda mapumziko zikiwa zimetoshana nguvu kwa kufungana bao 1-1, lakini dakika ya 75 kipindi cha pili, Bocco alirudi tena langoni mwa KMC na kutupia la pili katika mchezo huo ambao walionyesha kandanda la kuvutia.

Mtokea benchi, Ibrahim Ajibu alifanya kweli dakika ya 88 kwa kuifungia timu yake bao la tatu na kuifanya Simba kuibuka na ushindi wa mabao 3-1 ambayo yanaifanya kwa jumla siku ya jana kuvuna mabao 7-3 ukichanganya na ushindi wa asubuhi wa 4-3 dhidi ya Transit Camp.

Baada ya ushindi huo, kupitia mtandao wa instagram wa Simba iliandikaa "Full Time: Simba SC 3-1 KMC, Wachezee watoto sio sisi".

Mechi hiyo ni kipimo kizuri kwa Simba inayohitaji pointi 14 katika mechi 10 ilizobakiza msimu huu ili kutangazwa mabingwa, lakini pia KMC nayo ikihitaji kujiweka katika ukanda salama wa kuepuka kushuka daraja wakati huu ikiwa na pointi 33 katika nafasi ya 15 huku ikiwa imebakiza mechi tisa tu.

Katika mchezo huo, Simba iliwaanzisha Aishi Manula, Haruna Shamte, Gadiel Michael, Kennedy Juma, Pascal Wawa, Jonas Mkude, Hassan Dilunga, Said Ndemla, John Bocco, Luis Miquissone na Shiza Kichuya wakati benchi walikuwa Ally Salim, Yusufu Mlipili, Tairone Santos, Mzamiru Yassin, Francis Kahata, Ibrahim Ajibu na Cyprian Kipenye.

Kwa upande wa kikosi cha Simba kilichoanza dhidi ya Transit Camp jana asubuhi, kiliundwa na Beno Kakolanya, Shomari Kapombe, Mohammed Hussein 'Tshabalala', Yusuph Mlipili, Tairone Santos, Erasto Nyoni, Deo Kanda, Gerson Fraga, Meddie Kagere, Mzamiru Yassin na Rashid Juma.

Meneja wa Simba, Patrick Rweyemamu, juzi alisema kuwa wanatarajia kutafuta mechi zaidi ya mbili kadri zitakavyopatikana ili kuweza kuwapima zaidi wachezaji wao na kuwarejeshea utimamu wa mwili kama ilivyokuwa awali kabla ya Ligi Kuu kusimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

## Mkwasa sasa aona pa kuanzia Yanga

**Na Saada Akida**

KIPIGO cha mabao 3-0 ilichokipata Yanga kutoka kwa KMC FC juzi, kimeonyesha makosa yanayopaswa kufanyiwa kazi kabla ya kuelekea kuivaa Mwadui FC kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara itakayopigwa katika Uwanja wa Kambarage mkoani Shinyanga, kwa mujibu wa Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Boniface Mkwasa.

Katika mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam, Mkwasa ameliambia Nipashe kuwa pamoja na makosa ya kiufundi yaliyofanyika, Yanga ilizidiwa nguvu na kukosa stamina mambo ambayo yanamlazimu kuyafanyia kazi kabla ya kukutana na Mwadui FC katika mchezo wa Ligi Kuu Jumamosi wiki hii.

**Mkwasa ambaye aliiongoza timu hiyo kutokana na Kocha Mkuu, Mbelgiji Luc Eymael kuchelewa kurejea nchini, alisema ameona makosa mengi kwenye mchezo huo ikiwamo wachezaji kutokuwa na utimamu wa mwili pamoja na kufanya makosa ya kizembe.**

Alisema mechi hiyo wamepoteza ila imempa mwanga wa kuona nini anatakiwa kukifanya kabla ya kuanza kwa michezo ya Ligi Kuu na Kombe la FA watakapoivaa Kagera Sugar katika hatua ya robo fainali.

"Nimeona upungufu na tunahitaji kuongeza nguvu kwa wachezaji wangu, licha ya muda mdogo, nitajitahidi tuweze kufikia pale tunapotarajia kwenye program ya mazoezi tutakayoifanya kujiandaa dhidi ya Mwadui," alisema Mkwasa.

Wakati Mkwasa akieleza hayo, Kocha Msaidizi wa KMC FC, Habibu Kondo amesema ushindi dhidi ya Yanga unawapa morali wachezaji wao kuendelea kufanya vizuri katika michezo ijayo ya Ligi Kuu Bara.

KMC ipo katika nafasi ya 15 kwenye msimamo wa Ligi Kuu ikiwa tayari imeshacheza michezo 29 na kujikusanyia alama 33.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002